


MAMBO MUHIMU YANAYOHUSU MKATABA WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

2389

Ujue Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki



**MAMBO MUHIMU YANAYOHUSU MKATABA
WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

Ujue Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

*Watayarishaji:
Dk. Mohammed Omar Maundi
Tatu Tua, Adelardus Kilangi, Francis Imanjama*

FRIEDRICH EBERT STIFTUNG

Dar es Salaam 2002
© Friedrich Ebert Stiftung
East African Community
2002

ISBN 9987 22 036 3

Chapa na Ecoprint Ltd, email: ecoprint@raha.com

DIBAJI

Imeandikwa na **Mheshimiwa Amana Mushega, Katibu Mkuu, Jumuiya ya Afrika Mashariki**

Kwa niaba ya Sekretariati ya jumuiya ya Afrika Mashariki, napenda kukaribisha uchapishaji wa kitabu cha **Ujue Mkataba wa jumuiya ya Afrika Mashariki**. Chapisho hili linautambulisha Mkataba wa jumuiya kwa msomaji katika mtindo rahisi na unaovutia. Kitabu hiki pia kimeandikwa katika Kiswahili ambayo ni lugha inayaeleweka kwa wananchi walio wengi wa Afrika Mashariki.

Mkataba wa Kuanzishwa jumuiya ya Afrika Mashariki ulitiwa saina tarehe 30 Novemba, 1999 na kuanza kutumika rasmi tarehe 7 Julai, 2000 baada ya Nchi Washirika kuridhia mkataba huo.

Mkataba unaainisha maono ya kijasiri kuhusu hatima ya kuziunganisha Nchi Washirika yaoni Kenya, Uganda na Tanzania. Unayakinisha mfumo kamili wa ushirikiano baina ya Nchi Washirika katika Biashara, Uwekezaji na Maendeleo ya Viwanda; Sarafu na Sera za Fedha, Miundombinu na Huduma; Nguvu Kazi, Sayansi na Teknolojia; Utawanyaji usio na vikwazo wa nyenzo za uzalishaji; Kilimo na Uhakika wa Chakula, Mazingira na Usimamizi wa Mali Asili; Utalii na Usimamizi wa Wanyamapori.

Nyanja nyingine za ushirikiano zilizoinishwa katika Mkataba ni Shughuli za Afya, Kijamii na Kitamaduni; Nafasi ya Wanawake Katika Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi, Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi na jumuiya ya Kiraia; pamoja na ushirikiano katika masuala ya Sheria na Utoaji Haki: masuala ya kisiasa ikiwa ni pamoja na Ulinzi, Usalama na Mambo ya Nje. Mkataba pia unaeleza hatua mbalimbali katika maendeleo ya mfungamano kama vile uanzishaji wa Muungano wa Forodha, ambao ni mlango muhimu katika shughuli za jumuiya, kisha baadaye Soko la Pamoja, likifuatiwa na Muungano wa Sarafu na hatimaye Shirikisho la Kisiasa la Dola za Afrika Mashariki.

Pamoja na kusimika vyombo vya mamlaka za jumuiya ambavyo ni pamoja na Mkutano wa Wakuu wa Nchi, Baraza la Mawaziri, Kamati ya Uratibu, Kamati za Kisekta, Mahakama ya Afrika Mashariki, Bunge la Afrika Mashariki, na Sekretariati, Mkataba pia unasisitiza ushiriki wa Sekta Binafsi na jumuiya ya Kiraia katika mwenendo mzima wa mfungamano.

Mkataba umetilia maanani maslahi ya eneo hili la Afrika Mashariki. Inaeleweka kwamba mataifa madogo, na dhaifu hayana mustakbali murua katika ulimwengu huu wa ushindani mkubwa. Kwa kuwezesha kuwapo kwa soko pana zaidi, Jumuiya itasaidia kukuza biashara na uwekezaji katika eneo hili. Ushirikiano katika kukuza sayansi na teknolojia utatusaidia kwenda na wakati na kuongeza kasi ya ukuaji viwanda na hivyo kuongeza ajira na kubaresha hali za maisha ya watu Kwa ujumla, Jumuiya itaongezea fahari, hadhi na kujiamini, tena itaboresha nafasi yetu katika mahusiano na jamii nyingine duniani.

Mkataba huu ni hati ya msingi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiainisha maono, malengo, mifumo, miundo na mikakati ya mfungamano wa nchi za eneo hili.

*Uefewa mzuri wa Mkataba ndiyo mwanzo wa wananchi kuwezo kushiriki katika mwenendo mzima wa mfungamano katika enea letu hili. Napendekeza kwamba **Ujue Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki** kisomwe kwa bidii Afrika Mashariki kote. Napenda kutoa shukrani kwa Shirika la Friedrich Ebert kwa msaada wake mkubwa uliowezesha kutolewa kwa kitabu hiki ambacho kitasaidia sana kueneza uelewa wa malengo na majukumu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.*

*Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Arusha, Tanzania
juni, 2002*

Saalam za Shirika la Friedrich Ebert

Kabla ya kusainiwa kwa Mkataba wa Uanzishaji wa jumuiya ya Afrika Mashariki hapa Novemba 30, 1999, Shirika la Friedrich Ebert lilishiriki katika kuandaa miradi mbali mbali iliyokuwa na uhusiano wa karibu wa uanzishwaji wa Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki. Ushiriki huu ulitokana na kutambua na kuthamini umuhimu, madhumuni na malengo ya ushirikiano baina ya wananchi wa Afrika Mashariki.

Baada ya kufufuliwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Shirika la Friedrich Ebert bado lina ari ya kuendelea kushirikiano na nchi tatu za Afrika Mashariki zinazounda jumuiya hiyo, pamoja na watu wake, katika uhamasishaji na uimarishaji wa Jumuiya mpya.

Utayarishaji wa kitabu hiki ni moja ya juhudi hizo. lengo lake kubwa ni kuwahamasisha wananchi wa Afrika Mashariki ili waweze kuelewa kuwapo kwa jumuiya, madhumuni yake na jinsi watakavyoweza kushiriki na kufaidika katika utekelezaji wa malengo yake.

Ni matumaini yetu kuwa kitabu hiki kitatumika shuleni, vyuoni, kwenye mafunzo ya Elimu ya Watu Wazima, kwenye mashirika yasiyo ya kiserikali, kwenye ofisi za serikali na hata na wananchi wa kawaida.

Katika utayarishaji wa chapisho hili, watu wengi wametoa msaada wao kwetu. Ningependa kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwao nikitarajia kuwa kazi hii muhimu itakidhi malengo yaliyokusudiwa.

Ahsanteni sana.

Peter Haeussler

Mkurugenzi Mwakilishi

Shirika la Friedrich Ebert

Dar es Salaam, Tanzania.

DIBAJI.....	I
MWONGOZO	1
1.UTANGULIZI	3
1.1. SURA YA KWANZA: TAFSIRI	5
1.1.1 SURA YA PILI: UANZISHAJI NA MISINGI YA JUMUIYA	10
2. VYOMBO VYA JUMUIYA NA UTAWALA	11
2.1 SURA YA TATU: UANZISHAJI WA VYOMBO VYA JUMUIYA.....	11
2.1.1 SURA YA NNE: MKUTANO WA WAKUU WA NCHI.....	12
2.1.2. SURA YA TANO:BARAZA LA MAWAZIRI.....	13
2.1.3 SURA YA NANE: MAHAKAMA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI	13
2.1.4 SURA YA TISA: BUNGE LA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI	15
2.1.5 SURA YA KUMI: SEKRETARIETI NA WAFANYAKAZI WA JUMUIYA	19
2.1.5 SURAYA ISHIRINI NA NANE: MASUALA YA FEDHA	20
3. USHIRIKIANO KATIKA UCHUMI, BIASHARA NA MALIASILI.....	22
3.1 SURA YA KUMI NA MOJA: USHIRIKIANO KWENYE ULEGEZAJI MASHARTI NA MAENDELEO YA BIASHARA.	22
3.1.1 SURA YA KUMI NA MBILI: USHIRIKIANO KATIKA UWEKEZAJI NA MAENDELEO YA VIWANDA.....	22
3.1.2 SURA YA KUMI NA NNE: USHIRIKIANO KATIKA HAZINA YA SERIKALI NA FEDHA	23
3.1.3 SURA YA KUMI NA SABA: UHAMAJI HURU WA WATU, NGUVUKAZI, HUDUMA NA HAKI YA KUANZA MASKANI NA MAKAZI.....	24
3.1.4.SURA YA KUMI NA NANE: KILIMO NA UHAKIKA WA CHAKULA.....	25
3.1.5 SURA YA KUMI NA TISA: USHIRIKIANO KWENYE MAZINGIRA NA MALIASILI.....	28
3.1.6 SURA YA ISHIRINI: USHIRIKIANO KWENYE USIMAMIZI WA UTALII NA WANYAMA PORI	28
3.1.7 SURA YA ISHIRINI NA TANO: SEKTA BINAFSI NA RAIJA	29
4.HUDUMA, VIWANGO NA MASUALA YA KIJAMII	31
4.1 SURA YA KUMI NA TANO: USHIRIKIANO KATIKA MIUNDOMBINU NA HUDUMA	31
4.1.1 SURA YA KUMI NA SITA: USHIRIKIANO KATIKA MAENDELEO YA WATU , SAYANSI NA TEKNOLOJIA	34
4.1.2 SURA YA ISHIRINI NA MOJA: MASUALA YA AFYA, JAMII NA UTAMADUNI	35
4.1.3 SURA YA ISHIRINI NA MBILI: KUIMARISHA NAFASI YA WANAWAKE KATIKA MAENDELEO YA KIUCHUMI NA KIJAMII	36
5.MASUALA YA SIASA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA	36
5.1. SURA YA ISHIRINI NA TATU: USHIRIKIANO KATIKA MASUALA YA KISIASA.....	36
5.1.1 SURA YA ISHIRINI NA SITA:UHUJIANO NA MASHIRIKA MENGINE YA KIKANDA NA YA KIMATAIFA NA WAHISANI.....	38
6. MENGINEYO.....	38
6.1 SURA YA ISHIRINI NA TISA: VIFUNGU VYA JUMLA, VYA MPITO NA VYA MWISHO	38
7.VIAMBATISHO	40
7.1 HATI ZA AWALI ZA MKATABA WA UANZISHAJI WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI.....	40
7.1.1 BUNGE LA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI KATIKA KIKAO CHAKE CHA KWANZA – NOVEMBA 29 2001	42
7.1.2 MAHAKAMA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI	43

MWONGOZO

Kitabu hiki ni muhtasari wa Chapa ya Kiswahili ya Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliosainiwa Novemba 30, 1999. Tofauti na Chapa ya Kiswahili ya Mkataba wa Jumuiya ambayo imetayarishwa katika lugha na muundo wa kisheria, kitabu hiki kimetayarishwa katika Kiswahili simulizi fasaha na chepesi ili kuwasaidia wasomaji wa kawaida kuwezo kuelewa Mkataba bila ya matatizo yoyote.

Walengwa wa kitabu hiki ni makundi mbalimbali ya jamii ya watu wa Afrika Mashariki, hasa, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari. Kinaweza kutumika pia kwa elimu ya watu wazima na katika mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Lengo kubwa la kitabu hiki ni kuhamasisha wananchi wa Afrika Mashariki kuwezo kuelewa kuwapo kwa jumuiya ya Afrika Mashariki, madhumuni yake na jinsi watakavyoweza kushiriki na kufaidika katika utekelezaji wa malengo ya jumuiya.

Mpangilio wa kitabu hiki unatofautiana na ule wa Chapa ya Kiswahili ya Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa namna moja kubwa. Nayo ni kwamba wakati mpangilio wa chapa ya Kiswahili ya Mkataba wa Jumuiya unaanza na sura na ibara zinazofuata , yaani sura ya kwanza mpaka ya mwisho (Sura ya kwanza mpaka ya 29), na ibara ya kwanza mpaka ya mwisho (Ibara ya kwanza mpaka ya 153), sura na ibara katika kitabu hiki zimepangwa kwenye maeneo sita yenye vichwa vya habari vinavyotofautiana.

Eneo la kwanza ni la utangulizi ambalo linajumuisha sura ya kwanza na ya pili. Sura ya kwanza inatoa tafsiri na ya pili ni juu ya uanzishaji wa misingi ya Jumuiya.

Eneo la pili ni lile linalojumuisha sura zinazohusu vyombo vya Jumuiya na utawala. Vyombo hivi vinafafanuliwa katika sura ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita, ya saba, ya nane, ya tisa, ya kumi na ya ishirini na nane.

Eneo la tatu linohusu ushirikiano katika uchumi, biashara na maliasili. Sura zinazokamilisha eneo hili ni pamoja na sura ya kumi na mbili, ya kumi na nne, ya kumi na saba, ya kumi na nane, ya kumi na tisa, ya ishirini na ya ishirini na tano.

Eneo la nne linahusu viwango na masuala ya kijamii. Linajumuisha sura za kumi na tano, kumi na sita, ishirini na moja, na ya ishirini na mbili.

Eneo la tano ni la masuala ya siasa na ushirikiano wa kimataifa. Linajumuisha sura ya ishirini na tatu na ya ishirini na sita.

Eneo la sita ni juu ya mengineyo ambalo muhimili wake ni sura ya ishirini na tisa inayohusu vifungu vya jumla, vya mpito na vya mwisho.

Eneo la saba na la mwisho ni la vielelezo. Linahusu michoro mbalimbali iliyomo kwenye kitabu hiki ambayo ni vielelezo vya ujumbe uliomo kwenye sura za maeneo mengine sita.

Kutokana na mpangilio wa sura mbalimbali katika maeneo sita, ni dhahiri kwamba moja ya mapungufu ya kitabu hiki ni kwamba hakiwakilishi sura na ibara zote zilizomo katika Chapa ya Kiswahili ya Mkataba wa Jumuiya. Hata hivyo, tahadhari imechukuliwa kuhakikisha kwamba mapungufu haya hayapotezi tafsiri, maana, madhumuni, malengo na mwelekeo wa Jumuiya.

1. UTANGULIZI

Nchi tatu za Afrika Mashariki, yaani Kenya, Uganda na Tanzania, zina historia ndefu ya ushirikiano wa kiutamaduni, kijamii na kiuchumi. Ingawa hapo nyuma ushirikiano huu ulianzishwa kwa faida ya utawala wa kikoloni wa Kiingereza, ushirikiano huo wa kikoloni ndio uliojenga msingi, wa ushirikiano mpya wa baadaye wa nchi huru za Afrika Mashariki.

Kufuatia kupata uhuru kwa nchi zote tatu katika nusu ya kwanza ya miaka ya 1960 maslahi ya kiutamaduni, kijamii na kiuchumi ndiyo yamekuwa nguzo ya ushirikiano baina ya nchi hizi za Afrika Mashariki.

Taasisi ya kwanza iliyoungwa na nchi huru za Afrika Mashariki kusimamia ushirikiano baina yao ni jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ilianzishwa mwaka 1967 Makao Makuu ya jumuiya hiyo yalikuwa Arusha, Tanzania. Kwa bahati mbaya jumuiya hiyo ilivunjika mwaka 1977

Kuvunjika kwa jumuiya hiyo kulitokana na sababu nyingi. Mojawapo ni tofauti za kisiasa, kiitikadi na mifumo ya uchumi baina ya nchi wanachama. Kwa mfano, wakati Kenya iliendelea na mfumo wa uchumi huria iliourithi kutoka katika uchumi wa kikoloni, Uganda na Tanzania zilianzisha mifumo mipya ya uchumi uliomilikiwa na Serikali.

Sababu nyingine zilizochangia kuvunjika kwa Jumuiya ya Afriku Mashariki ni pamoja na ukosefu wa utashi wa kisiasa baina ya viongozi, kutoshiriki kikamilifu kwa sekta binafsi na raia kwenye shughuli za ushirikiano, na kutokuwapo kwa usawa katika kugawana matunda ya Jumuiya baina ya Nchi Wanachama. Hali hii ilisababishwa na tofauti ya viwango vya maendeleo baina ya Nchi Wanachama. Wakati Kenya iliendelea kiviwanda, Uganda na Tanzania zilikuwa ni soko kwa bidhaa zilizokuwa zikizalishwa Kenya. Kutokuwapo na sera maalum za kurekebisha tofauti hizi kulichangia, kwa kiasi kikubwa, kuvunjika kwa Jumuiya ya kwanza ya Afrika Mashariki.

Kufuatia kuvunjika kwa jumuiya mwaka 1977, Nchi Wanachama ziliajiri mpatanishi ambaye alihusika katika kugawa mali na madeni ya jumuiya baina ya Nchi Wanachama. Kazi hii ilifanyika katika kipindi cha miaka saba, yaani toka 1978 mpaka 1984, wakati Nchi Wanachama walipoweka saina Makubaliano ya Upatanishi. Makubaliano ya Upatanishi yalisainiwa Arusha, Tanzania, Mei 24, 1984.

Miongoni mwa vipengele vya Makubaliano ya Upatanishi, kimojawapo kilikuwa ni makubaliano ya kuangalia upya maeneo ambayo nchi za Afrika Mashariki zingeweza kushirikiana tena katika siku za baadae. Imechukua zaidi ya miaka kumi kuamua maeneo mapya na kuunda taasisi nyingine ya ushirikiano.

Juhudi hizi zilianza na makubaliano ya Novemba 30, 1993 ya kuanzisha Tume ya Kudumu ya Ushirikiano ili ihusike na uratibu wa masuala ya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiusalama na kisiasa. Makubaliano ya uanzishaji wa Sekretariati ya Tume ya kudumu ya Ushirikiano yalitiwa saina Novemba 26, 1994.

Baada ya kutathmini hatua zilizochukuliwa na Tume katika kuendeleza ushirikiano, viongozi wa Afrika Mashariki walifikia uamuzi, huko Arusha, Tanzania, wa kuanzisha

tena Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki. Hivyo waliagiza Tume kushughulikia majadiliano juu ya Mkataba wa Jumuiya hiyo mpya ya Afrika Mashariki.

Matayarisho ya ufufuaji wa Jumuiya mpya yalikamilika mwaka 1999. Mkataba wa Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki ulisainiwa na viongozi wa nchi za Afrika Mashariki Arusha, Novemba 30, 1999. Mkataba huu tayari umesharidhiwa na nchi zote tatu wanachama. Vyombo vyote muhimu vinavyotajwa katika Ibara ya 9 ya Mkataba tayari vimeshaundwa.

1.1. SURA YA KWANZA: TAFSIRI

Katika Mkataba huu:

Sheria ya Jumuiya ina maana sheria ya Jumuiya kulingana na Mkataba huu;

Tume ya Ukaguzi ina maana ya Tume ya Ukaguzi iliyoanzishwa na Ibara ya 134 ya Mkataba huu;

Bunge ina maana Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki lililoanzishwa na Ibara ya 9 ya Mkataba huu;

Muswada ina maana ya Muswada wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki;

Jamii ya watu ina maana ya mkusanyiko wa maisha ya kijamii ya hiyari, yenye kutawaliwa na taratibu za kisheria za wakazi wote;

Katibu wa Bunge ina maana ya Katibu wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki aliyeteuliwa chini ya Ibara ya 48 ya mkataba huu;

Msafirishaji wa kawaida inajumuisha mtu au shughuli ya biashara ya kutoa huduma ya kusafirisha mizigo au abiria, kwa kukodi au kwa tuzo na anayefanya kazi chini ya sheria ya Nchi Wanachama;

Ushuru wa Forodha kwa Nchi zisizo Wanachama ina maana viwango sawa vya ushuru vinavyowekwa kwa bidhaa toka nchi ambayo sio mwanachama;

Soko la pamoja ina maana masoko ya Nchi Wanachama yataunganishwa kuwa soko moja ambapo kutakuwa na uhuru wa kuhamisha mtaji, nguvu kazi, bidhaa na huduma;

Hati sawa za kusafiria ina maana ya pasipoti au hati yoyote inayafao kwa kusafiria itakayatambulisha mwenye hati hiyo, iliyotolewa na au kwa niaba ya Nchi Mwanachama ambayo mhusika ni raia na itajumuisha pasi za kusafiria baina ya nchi na nchi;

Jumuiya ina maana Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoanzishwa katika Ibara ya 2 ya Mkataba huu; ***Pande zinazoweka Mkataba*** ina maana ya Jamhuri ya Kenya, Jamhuri ya Uganda na Jamhuri ya Muungana wa Tanzania; .

Ushirikiano unajumuisha shughuli za Nchi Wanachama zinazafanywa kwa pamoja, au shughuli zote zinazofanywa kwa kushirikiano ili kuendeleza malengo ya Jumuiya kama yalivyoonyeshwa chini ya Mkataba huu au mkataba wowote au makubaliano yaliyafanywa chini ya mahusiano na malengo ya Jumuiya;

Kamati ya Uratibu ina maana Kamati ya Uratibu ya Jumuiya iliyoanzishwa kutokana na Ibara ya 9 ya Mkataba huu;

Baraza la Mawaziri ina maana ya Baraza la Mawaziri la Jumuiya lililoanzishwa kutokana na Ibara ya 9 ya Mkataba huu;

Mshauri wa Jumuiya ina maana ya Mshauri wa Jumuiya kama ilivyotolewa katika Ibara ya 69 ya Mkataba huu;

Ushuru msawazisho ina maana kadi inayatazwa bidhaa yoyote inayoingizwa nchini kwa lengo la kusawazisha moja kwa moja au vinginevyo ruzuku iliyotolewa kwa mtengenezaji, kwa mazao au kwa kusafirisha nie bidhaa hiyo;

Mahakama ina maana mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoanzishwa kutakana na Ibara ya 9 ya Mkataba huu;

Wakala wa ushuru wa forodha ina maana mtu aliyepewa leseni katika nchi mojawapo Mwanachama kutoa huduma kwa kutoza ada, kwa ajili ya hati na ulipaji ushuru wa bidhaa ziingiazo na zitakazo;

Shirika la Ndege lililoteuliwa ina maana shirika la ndege lililoteuliwa na kupata kibali cha mamlaka ya Nchi Wanachama ili kutoa huduma zilizokubalika;

Marejesho ina maana kiasi cha ushuru au kadi ya kuingiza bidhaa inayorejeshwa au kusamehewa kwa bidhaa zilizothibitishwa kuwa tayari zimesafirishwa;

Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda wa Afrika Mashariki ina maana ya mkakati uliotolewa chini ya Ibara ya 80 ya Mkataba huu;

Taarifa za kisheria za Afrika Mashariki ina maana ya ripoti za hukumu zilizotolewa na Mahakama ya Rufaa ya zamani ya Afrika Mashariki na Mahakama Kuu za Kenya, Tanzania na Uganda;

Mjumbe aliyechaguliwa ina maana mjumbe wa Bunge aliyechaguliwa chini ya Ibara ya 50 ya Mkataba huu;

Mazingira ina maana maliasili ya hewa, maji, udongo, mimea na wanyama, mifumo ya ikolojia, ardhi na mandhari yaliyotengenezwa na binadamu, urithi wa utamaduni, vipengele vya mandhari na maingiliano ya kiuchumi-jamii na viumbe vinavyoishi na vile visivyoishi;

Mgawanyo wa haki wa mafao ina maana ya mgawanyo wa mafao unaostahili kulingana na mchango wa nchi;

Mwaka wa fedha ina maana mwaka wa fedha uliotajwa chini ya Ibara 132 ya Mkataba huu;

Nchi ya Kigeni ina maana Nchi yoyote mbali na Nchi Wanachama

Msafirishaji mizigo ina maana mtu yoyote anayejihusisha kwa malipo, ama kama wakala wa wasafirishaji wengine au kwa kujihusisha mwenyewe katika uendeshaji wa huduma za usafiri na shughuli za utoaji mizigo;

Gazeti ina maana Gazeti rasmi la Jumuiya;

Jinsia ina maana ya nafasi ya wanawake na wanaume katika jamii;

Mkuu wa Serikali ina maana ya mtu aliyetajwa hivyo na Katiba ya Nchi Mwanachama;

Mkuu wa Nchi ina maana mtu aliyetajwa hivyo na Katiba ya Nchi Mwanachama;

Kuingiza bidhaa pamoja na fasili tofauti zinazoweza kutokea, hapa itamaanisha kuleta au kusababisha kuleta ndani ya Nchi Wanachama bidhaa toka nchi ya kigeni;

Mrajisi mali mwenyeji ina maana ya raia mfanyabiashara wa Nchi Mwanachama lakini ambaye hana uraia wa nje;

Taasisi za Jumuiya ina maana ya taasisi za Jumuiya zilizoanzishwa na Ibara ya 9 ya Mkataba huu

Viwango vya kimataifa ina maana viwango vinavyotumiwa kimataifa au na mashirika ya viwango yaliyopo katika nchi;

Jaji ina maana ya Jaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki ikiwa na Rais na Naibu Rais wa Mahakama hiyo;

Hukumu itakuwa pamoja na uamuzi, maoni, amri, agizo, au hukumu ya mahakama;

Waziri kuhusiana na Nchi Wanachama ni mtu aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Serikali ya Nchi Mwanachama na mtu mwingine yeyote yule, licha ya cheo chake, ambaye, kufuatana na sheria yoyote ya Nchi Mwanachama anatenda kazi za Waziri katika Nchi hiyo;

Usafirishaji kwa Njia Mbalimbali ina maana usafirishaji wa bidhaa au huduma kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa kutumia njia mbili au zaidi za usafirishaji wa msingi wa mkataba mmoja uliotolewa na mtu anayeshughulikia huduma hizo, wakati huohuo mtu huyo huchukua jukumu la kukamilisha shughuli hiyo;

Huduma za Usafirishaji kwa njia mbalimbali inajumuisha vifaa kama vya kubebea uzito mkubwa, kreni za dela pacha, kreni za mihimili, lifti, vifaa vikubwa vya kubebea mizigo, maghala yanayoendeshwa kwa mitambo, vifaa vya kushushia mizigo, huduma za usafiri, vibeebea, mizigo vya chini, kreni zinazotembea, kreni mihimili za kantena, fakalifti za uzito mkubwa, matrela makubwa, hanamu zinazabebeka, mabehewa makantena, mabehewa maalumu na malori kwa ajili ya makantena, matolori kwa ajili ya bidhaa tofauti;

Mabunge ya kitaifa pamoja na tofauti za kisarufi na matamshi yanayolingana inamaanisha mabaraza ya kutunga sheria ya nchi yaliyoundwa na Nchi Wanachama;

Vizuizi visivyo vya ushuru wa forodha ina maana mahitaji ya kiutawala na kiufundi yanayowekwa na Nchi Mwanachama katika usogezaji wa bidhaa;

Vyombo vya Jumuiya ina maana ya vyombo vya jumuiya vilivyoanzishwa na Ibara ya 9 ya Mkataba huu;

Gharama nyingine zenye athari sawa ina maana kadi yoyote, kodi ya ziada, kodi ya maendeleo au gharama inayotozwa kwa kuingiza bidhaa na siyo kwa bidhaa zinazofanana zilizozalishwa ndani na haijumuishi ada na gharama za aina hiyo zinazohusiana na gharama za huduma zilizotolewa;

Nchi Wanachama ina maana Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Kenya, Jamhuri ya Uganda na nchi nyingine yoyote itakayopewa uanachama wa Jumuiya chini ya Ibara ya 3 ya Mkataba huu;

Mtu ina maana mtu kwa asili au kwa sheria;

Rais wa Mahakama ina maana mtu aliyeteuliwa kuwa Rais wa Mahakama chini ya Ibara ya 24 ya Mkataba huu;

Kanuni ya kutawiana ina maana kanuni inayozingatia tofauti katika utekelezaji wa hatua za kufanikisha madhumuni ya pamoja ya uunganishaji wa shughuli za kiuchumi;

Kanuni ya Kukamilishana ina maana kanuni ambayo inaelezea kiwango ambacho vitu mbalimbali vya uchumi vinasaidiana katika shughuli za uchumi;

Kanuni ya Usaidizi ina maana kanuni inayosisitizia ushirikiano wa washiriki katika viwango mbalimbali kwa mapana na marefu katika njia ya kuunganisha uchumi;

Kanuni ya vibadilika vya kijiometri ina maana kanuni ya uwezo wa kubadilika inayaruhusu kuendelea katika ushirikiano kati ya kundi dogo la wanachama kwenye mpango mkubwa uliunganishwa ndani ya maeneo mbalimbali na katika kasi yake tofauti;

Sekta binafsi ina maana sehemu ya uchumi ambayo haimilikiwi au kudhibitiwa moja kwa moja na Dola;

Hati ya Awali ina maana ya makubaliano yoyote yanayoongezea, kurekebisha au kuthibitisha Mkataba huu;

Mrajisi ina maana ya Mrajisi wa Mahakama iliyoteuliwa chini ya Ibara ya 45 ya Mkataba huu;

Hatua za tahadhari ina maana hatua za kusalimisha uchumi zinazochukuliwa na Nchi Mwanachama kama inavyotolewa chini ya Ibara ya 78 na 88 ya Mkataba huu;

Mishahara na Masharti mengine ya Utumishi inajumuisha ujira, malipo ya kazi ya ziada, mishahara, taratibu za ujira, likizo, safari, usafiri kwa ajili ya likizo, pensheni na mafao mengine ya kustaafu, kupunguzwa na kuacha kazi, saa za kazi, kupanda cheo, matibabu, nyumba, mipango ya safari za kikazi na marupurupu;

Sekretariati ina maana Sekretariati ya Jumuiya kama ilivyoanzishwa kwenye Ibara ya 9 ya Mkataba huu;

Katibu Mkuu ina maana Katibu Mkuu wa Jumuiya kama inavyotajwa katika Ibara ya 67 ya Mkataba huu;

Kamati ya Kisekta ina maana kamati ya kisekta iliyoanzishwa katika Ibara ya 20 ya Mkataba huu; **Baraza la Kisekta** ina maana Baraza la Kisekta chini ya Ibara ya 14 ya Mkataba huu;

Huduma ina maana huduma zinazotolewa kwa malipo ambapo zipo chini ya vifungu vinavyohusika na uhuru wa kusogeza bidhaa, mtaji au watumishi; **Wakala wa Meli** ina maana mwakilishi wa nchini anayeiwakilisha kampuni ya meli;

Spika wa Bunge ina maana ya Spika wa Bunge kama ilivyotajwa katika Ibara ya 53 ya Mkataba huu;

Ruzuku ina maana mchango wa fedha wa Serikali au shirika lolote la umma ndani ya enea la Nchi Mwanachama au pale ambapo kuna aina fulani ya uchangiaji wa kipato au bei kwa maana ya Ibara ya 16 ya Mkataba wa jumla wa kimataifa kuhusu ushuru wa forodha na biashara (GATT 1994);

Mkutano wa Wakuu wa Nchi ina maana mkutano wa Wakuu wa Nchi ulioanzishwa na Ibara ya 9 Mkataba huu;

Taasisi za Jumuiya ya zamani ya Afrika Mashariki zinazoendelea kudumu ina maana na inajumuisha Chao cha Wanaonga cha Afrika Mashariki, Soroti, Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki, Chao cha Ukutubi cha Afrika Mashariki na Baraza la Vyao Vikuu vya Afrika Mashariki;

Mawasiliano ya Anga ina maana aina yoyote ya utumiaji, utaoji au upakeaji maondishi, piaha na sauti au habari yoyote kwa waya, radio, kwa macho au mifumo-mingineyo ya magneta;

Jumuiya ina maana Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoanzishwa katika Ibara ya 2 ya Mkataba huu; **Taratibu za Biashara** ina maana shughuli zinazohusiana na ukusanyaji, uwekaji, utaoji na usambazaji wa takwimu na habari kuhusu shughuli zote zinazohusu biashara ya kimataifa;

Mkataba ina maana Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki na marekebisho yoyote yatakayofanyika. Katika Mkataba huu, kurejea kwenye sheria au Hati ya Awali kutafasiriwa kama marejeo ya kwenye sheria au Hati ya Awali kama itakavyofanyiwa marekebisha ya mara kwa mara, kuongezwa au kubadilishwa.

1.1.1 SURA YA PILI: UANZISHAJI NA MISINGI YA JUMUIYA

Sura ya Pili inajumuisha Ibara ya mpaka ya 8. Pamoja na uanzishwaji wa Jumuiya yenyewe ***Ibara ya Pili inahusu uanzishwaji wa Muungano wa forodha wa Afrika Mashariki na Soko la pamoja. Ibara ya 3 inahusu muundo wa Jumuiya.*** Kibali na kutaja nchi tatu za Afrika Mashariki kama wanachama waanzilishi, inagusia uwezekano, sifa na masharti kwa nchi nyingine kuwezo kuwa wanachama wa Jumuiya. Sifa na masharti haya ni pamoja na nchi inayataka kuwa mwanachama kuikubali Jumuiya kama ilivyowekwa katika Mkataba, kukubali kanuni za demokrasia, utawala wa sheria na haki za binadamu, mchango madhubuti wa nchi inayotaka kuwa mwanachama katika uimarishaji ushirikiano; ujirani bora; uanzishaji na uendelezaji wa soko huria, na kukubaliana kwa sera za kiuchumi na kijamii baina ya wanachama na nchi inayotaka kujiunga.

Ibara ya 4 inahusu uwezo wa kisheria wa Jumuiya. Mbali na kuwa na hadhi ya kuwa chombo cha ushirikiano, Jumuiya itakuwa na uwezo wa kupata, kumiliki, kutumia na kuuza ardhi na mali nyingine. Itaweza kukopa, kushitaki na kushitakiwa pia. Katibu Mkuu ndiye atakayekuwa mwakilishi wa Jumuiya.

Ibara ya 5 inataja madhumuni ya Jumuiya, ambayo ni pamoja na kuunda sera na pragramu zinazolenga katika kuendeleza ushirikiano katika nyanja za siasa, uchumi, jamii, utamaduni, ulinzi, usalama, sheria na shughuli za mahakama. Katika kutimiza madhumuni haya, Nchi Wanachama zinakubaliana kuchukua hatua za kuanzisha muungano wa faradha, Soko la pamoja, na baadae, muungano wa kifedha na hatimaye Shirikisho la Kisiasa ili kuimarisha na kusimamia ushirikiano wa viwanda, biashara, miundombinu, utamaduni, jamii na siasa.

Ibara ya 6 inahusu misingi muhimu ya Jumuiya, ambayo ni pamoja na kuaminiana, ridhaa ya kisiasa na usawa wa dola, kuishi pamoja kwa amani na ujirani mwema, utatuaaji wa migogoro kwa niia ya amani, utawala mzuri, ugawanaji wa haki wa mafao na ushirikiano kwa manafao ya wate.

Ibara ya 7 inahusu misingi ya utekelezaji ya Jumuiya, ambayo ni pamoja na ushirikiano unaoendeshwa na watu wenyewe kwa utaratibu wa Soko huria, uandalizi wa sera zinazovutia na miundombinu bora, uanzishaji wa sera za kiuchumi. zitakazosaidia uzalishaji wa bidhaa za kuuza nje, kufuata kanuni ya kusaidiana; na ugawanaji wa haki wa faida itokanayo na shughuli za Jumuiya.

Ibara ya 8 inahusu hatua za jumla za utekelezaji.



2. VYOMBO VYA JUMUIYA NA UTAWALA

2.1 SURA YA TATU: UANZISHAJI WA VYOMBO VYA JUMUIYA

Ibara ya 9 inahusu uundaji wa, Vyombo na taasisi za jumuiya. Vyombo vya Jumuiya ni zile idara na vitengo mbalimbali vya Jumuiya. Kila chombo kina majukumu yake maalum. Vyombo hivi vinapewa uwezo na majukumu kutaka jumuiya yenyewe. Mkutano wa Wakuu wa Nchi unaweza kuanzisha chombo kingine kipya.

jumuiya imeanzisha vyombo vifuatavyo kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali:


- Mkutano wa Wakuu wa Nchi
- Baraza la Mawaziri
- Kamati ya Uratibu
- Kamati za Sekta
- Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki
- Bunge la Afrika Mashariki
- Sekretarieti

2.1.1 SURAYA NNE: MKUTANO WA WAKUU WA NCHI

Sura hii inajumuisha Ibara ya 10 mpaka Ibara ya 12.

Ibara ya 10 inahusu muundo wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi. Mkutano huu utawahusisha viongozi ambao ni wakuu wa nchi au wakuu wa serikali za Nchi Wanachama. Kwa sasa hivi, wakuu hawa ni Maraisi wa Nchi Wanachama, yaani Rais wa Kenya, Tanzania na Uganda.

Ibara ya 11 na ya 12 zinahusu kazi za Mkutano wa Wakuu wa Nchi. Mkutano wa Wakuu wa Nchi ndio utakuwa unatao maelekezo ya jumla kwa jumuiya. Hata hivyo, wakuu hawa wa nchi wanaweza kukasimu madaraka yao kwa maafisa au Vyombo vingine.



Mkutano wa Wakuu wa Nchi ndio utakaokuwa ukitathmini hali ya amani na usalama katika eneo la Jumuiya. Utaangalia pia uwezekano wa kusonga mbele katika kuanzisha shirikisho la kisiasa.

Mkutano huu utakuwa ukiongozwa na mwenyekiti ambaye ni Rais wa mojawapo ya nchi za Afrika Mashariki. Uenyekiti huu utakuwa ukidumu kwa mwaka mmoja mmoja, na utakuwa na mzunguko kutaka nchi moja hadi nyingine miongoni mwa Nchi Wanachama.

Shughuli nyingine zitakazofanywa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi ni pamoja na kuteua Majaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki, kupokea wanachama wapya, au kukaribisha watazamaji.

2.1.2. SURA YA TANO:BARAZA LA MAWAZIRI

Sura hii inajumuisha Ibara ya 13 mpaka Ibara ya 16.

Ibara ya 13 inazingatia muundo wa Baraza la Mawaziri. Baraza hili litaundwa na mawaziri ambao watakuwa wamekwishateuliwa tayari na nchi zao kwa malengo ya ushirikiano wa kimataifa au kwa malengo ya ushirikiano wa Jumuiya.

Ibara ya 14 inahusu kazi za Baraza la Mawaziri ambazo zitakuwa ni pamoja na kutengeneza sera za Jumuiya. Baraza litakuwa pia na kazi ya kuangalia shughuli za kila siku za Jumuiya ikiwa ni pamoja na kukagua na kusimamia shughuli hizo. Baraza hili ndilo litakalokuwa na jukumu la kuangalia kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki inaendelea na shughuli zake kama kawaida. Baraza la Mawaziri litakutana mara mbili kwa mwaka.

2.1.3 SURA YA NANE: MAHAKAMA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

Sura hii inajumuisha Ibara ya 23 mpaka Ibara ya 47. Chanzo cha kuundwa kwa Mahakama ya Afrika Mashariki ni makubaliano ya Nchi Wanachama kuainisha mifumo ya sheria ya nchi zao. Uwezo wa mahakama hii utakuwa katika kupokea mashauri yatokanayo na mgongano katika mkataba huu wa ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mahakama itapokea pia mashauri ya masuala ya haki za binadamu.

Hata hivyo, kuwepo kwa Mahakama hii hakutaondoa uwezo wa mahakama za kitaifa katika Nchi Wanachama, ila itatumika kama sehemu ya rufaa, isipokuwa pale ambapo imetajwa waziwazi kuwa jambo fulani litakuwa chini ya Mahakama hiyo tu. Kwa vyovyote vile, Mahakama hii ndiyo itakuwa na haki zaidi ya kutafsiri Mkataba huu wa Afrika Mashariki kuliko mahakama za kitaifa.

Katika shughuli zake, Mahakama ya Afrika Mashariki itatumia lugha ya Kiingereza. Mahakama hii pia itakuwa na makao yake makuu ambayo yatapangwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi.

Ibara ya 24 inahusu uteuzi wa Majaji wa Mahakama.

Majaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki watateuliwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi. Kimsingi, wanapaswa kutoka katika Nchi Wanachama wa Jumuiya, yaani Kenya, Tanzania na Uganda. Majaji hawa wanapaswa kuwa waadilifu na kutopendelea upande wowote.

Idadi yao itakuwa si zaidi ya sita. Nchi Mwanachama haitatoa pendekezo la kuteua zaidi ya majaji wawili. Hii ina maana kuwa, kila nchi inaweza kutoa majaji wawili au zaidi. Lakini yule wa tatu au zaidi, anapaswa kuwa amependelekezwa na nchi nyingine mwanachama. Mahakama itaongazwa na Rais wa Mahakama na

Makamu Rais wa Mahakama. Urais huu utakuwa wa mzunguko katika Nchi Wanachama.

Ibara ya 28 mpaka 30 zinahusu Malalamiko kwenye Mahakama.



Mtu yeyote kutoka Nchi Mwanachama anaweza akapeleka malalamiko yake katika Mahakama hii.

Hata hivyo, malalamiko haya ni yale tu yenye nia ya kuhoji uhalali wa kanuni, agizo, uamuzi au kitendo chochote cha Nchi Mwanachama au chombo chochote cha Jumuiya na kutaka kuonyesha kuwa, kitendo kilichofanyika ni kinyume cha vifungu vya mkataba wa ushirikiano wa Afrika Mashariki. Malalamiko mengine yatakayoweza kupelekwa kwenye Mahakama hii ni yale yanayohusu migogoro kati ya wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya yenyewe.

Ibara ya 41 inahusu Mashitaka.

Mashitaka yanaweza kupelekwa katika Mahakama hiyo kwa maandishi au kwa mdomo. Walalamikaji katika Mahakama hiyo wanaweza kusimama wenyewe mahakamani au wakawakilishwa na mawakili au washauri wa kisheria. Mshauri huyo wa kisheria atakuwa na haki ya kufika mahakamani kila wakati shauri linapotajwa au kusikilizwa.

Ibara ya 38 mpaka 40 zinahusu Hukumu za Mahakama.

Moja ya hatua za kwanza ambazo Mahakama inaweza kuchukua katika uwezo wake wa hukumu ni kutoa amri za muda. Amri za muda au maagizo yoyote vinatumika kuzuia jambo fulani kuendelea kufanyika hadi Mahakama itakapotoa amuzi wa mwisho Pia, Nchi Wanachama zinaagizwa kuwa, mara mashauri yapelekwapo katika Mahakama hiyo, Nchi Wanachama zitaacha kushiriki katika kitendo chochote kile ambacho kinaweza kuharibu usuluhishi wa ubishani huo, au hata kuukuza zaidi.

Katika kutoa hukumu, Mahakama inaweza kutoa uamuzi au maamuzi ya awali ambayo hutangulia hukumu. Maamuzi ya awali sia hukumu kwa maana halisi ya hukumu, bali ni hatua ya Mahakama kueleza msimama wake juu ya kipengele fulani ambacho kinabishaniwa, na ambacho ni sehemu ya kesi nzima.

Baada ya kutolea Maamuzi vipengele vyote vinavyobishaniwa, na baada ya kupokea hoja za pande zote mbili, Mahakama itatao hukumu yake. Hukumu hii itakuwa ndiyo msimamo uliafikiwa na wengi wa majaji. Baada ya hukumu kutolewa, Nchi Mwanachama au Wanachama au vyombo husika vitakuwa na jukumu la kutekeleza maagizo ya hukumu hiyo.

Rufaa

Mahakama ya Afrika Mashariki haina utaratibu wa kukata rufaa kwenda mahakama nyingine tena. Hata hivyo, upande ambao haujuridhishwa na uamuzi uliutolewa unaweza kutoa maombi ili Mahakama iupitie tena uamuzi wake wa awali.

Hata hiyo, msingi mkubwa wa kupitia upya shauri fulani ni kugundulika kwa taorifa za kuaminika ambazo zingeweza kuathiri sana hukumu kama zingekuwa zimefahamika mahakamani wakati hukumu inatolewa. Pia, lazima ziwe hazikufahamika kwa sababu upande husika haukuwa katika nafasi ya kuzifahamu vema.

2.1.4 SURA YA TISA: BUNGE LA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

Sura hii inajumuisha Ibara ya 48 mpaka Ibara ya 65. Bunge la Afrika Mashariki ni chombo kinachaonzishwa ili kutekeleza majukumu ya kutunga sheria za Jumuiya.

Ibara ya 48 inahusu Muundo wa Bunge. Bunge litakuwa na wajumbe ishirini na saba wa kuchaguliwa na wajumbe watano ambao wataingia kwa nyadhifu zao. Hawa watakuwa ni pamoja na mawaziri wanaohusika na masuala ya ushirikiano wa Jumuiya. Katibu Mkuu wa jumuiya atakuwa pia ni sehemu ya Bunge.

Spika atakuwa na madaraka ya kumwalika mtu yeyote ambaye mchango wake utahitajika katika kujadili hoja yoyote iliyoletwa mbele ya Bunge.

Ibara ya 53 inahusu Spika wa Bunge.

Spika atachaguliwa kutokana na wajumbe wa Bunge. Cheo hiki kitashikwa kwa mzunguko kati ya Nchi Wanachama.

Ibara ya 49 inahusu Kazi za Bunge.

Mbali na wajibu wa kutunga sheria, Bunge la jumuiya litakuwa pia chombo cha kuendeleza mahusiano na mbunge ya kitaifa ya Nchi Wanachama kwa mambo yanayohusu jumuiya.

Bunge litakuwa na kazi ya kupitisha bajeti ya jumuiya. Kabla ya kupitisha bajeti, Bunge litaangalia na kutathmini ripoti za mpaka juu ya shughuli za Jumuiya. Kazi nyingine ya Bunge itakuwa ni kujadili mambo yote yanayohusu jumuiya na kupeleka mapendekezo kwenye Baraza la Mawaziri. Bunge litakuwa pia na kazi ya kupendekeza majina ya watu kwa ajili ya uteuzi wa nafasi za Katibu Mkuu na maofisa wengine wateule wa jumuiya.

Utaratibu wa Kutunga Sheria

Utungwaji wa sheria utanza kwa kupeleka muswada Bungeni. Ikiwa muswada utapitishwa na Bunge, Spika atapeleka kwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi ili wautolee kibali.

Muswada ukipitishwa na Bunge unaweza kukubaliwa au kukataliwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi. Iwapo utakataliwa, itabidi urudishwe tena Bungeni na kuomba Bunge lifanye marekebisha yoyote kadri itakavyokuwa imeambiwa.

Baada ya kuupitia kwa mara ya pili, Bunge litaurudisha tena kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi. Wakuu wa Nchi wakiukubali, unakuwa sheria. Wakiukataa utahesabika kuwa umepitwa na wakati.

Kupitishwa kwa muswada wa sheria na Wakuu wa Nchi unataka makubaliano ya Wakuu wote wa Nchi. Iwapo Mkuu mmoja wa Nchi atakataa, bado muswada huo hauwezi kupita.

Kanuni za Bunge

Bunge lina uwezo wa kutengeneza kanuni zake. Sheria na kanuni hizi zaweza kuhusiana na uwezo, haki, kinga ya wabunge na utaratibu wa uendeshaji wa shughuli zake.

Miswada ya kupeleka Bungeni inaweza kupendekezwa na mjumbe yeyote. Lakini miswada hii iwe inahusiana na shughuli za Jumuiya na sheria zilizoainishwa katika Mkataba wa Jumuiya.


Uchaguzi wa Wabunge

Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki watachaguliwa na Bunge la Taifa la kila Nchi Mwanachama. Kwa hiyo, kila anayetaka kugombea itabidi akapigiwe kura na Bunge la nchi yake.

Kila nchi itachagua wabunge tisa, ambao watakuwa siyo wabunge katika bunge la nchi husika. Uteuzi wa wabunge hao utaangalia uwiano wa uwakilishi wa vyama mbalimbali vya siasa vilivyoweza kuingia katika bunge la nchi husika. Uteuzi utaangalia pia jinsia na uwakilishi mwingine muhimu ulia katika kila Bunge la nchi, husika.

Sifa za kuchaguliwa kuwa Mbunge katika Bunge la Jumuiya:

- 1) Awe ni raia wa Nchi Mwanachama
- 2) Awe na sifa ya kuchaguliwa kuwa mbunge katika nchi yake kulingana na sheria na taratibu za nchi hiyo.
- 3) Asiwe na wadhifa wa uwaziri katika Nchi Mwanachama.
- 4) Asiwe mwajiriwa katika idara yoyote ya Jumuiya.
- 5) Awe na uzoefu au anathibitisha kupenda kuendeleza masuala ya Jumuiya.



2.1.5 SURA YA KUMI: SEKRETARIETI NA WAFANYAKAZI WA JUMUIYA

Sura hii inajumuisha Ibara ya 66 mpaka Ibara ya 73.

Sekretarieti ndiyo chombo mahsusi cha utendaji cha Jumuiya. Sekretarieti itakuwa na ofisi zifuatazo:

- Katibu Mkuu wa Jumuiya
- Manaibu wa Katibu Mkuu
- Mshauri wa Jumuiya
- Maofisa wengine

Katibu Mkuu atateuliwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi. Akisha kuteuliwa, nchi iliyomtoa Katibu Mkuu haitaweza kutoa Naibu Katibu Mkuu.

Katibu Mkuu atakuwa ndiye mtendaji mkuu wa Jumuiya. Yeye ndiye mkuu wa sekretarieti; ni afisa mhasibu mkuu wa Jumuiya, na katibu wa mikutano ya Wakuu wa Nchi: Atapewa pia kazi nyinginezo kadri inavyofao.

Manaibu Katibu Mkuu watakuwa kadhaa kulingana na majukumu. Hawa watateuliwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi, baada ya kupendekezwa na Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Wajibu mkubwa wa Manaibu Katibu Mkuu utakuwa ni kukaimu nafasi ya Katibu Mkuu na kufanya kazi nyinginezo kadri watakavyoagizwa na Baraza.

Mshauri wa Jumuiya

Mshauri wa Jumuiya ni mtu ambaye kazi yake kubwa ni kuishauri Jumuiya na idara zake zote juu ya masuala ya kisheria ya Jumuiya. Kazi zake zitapangwa na Baraza la Mawaziri la Jumuiya. Atakuwa na uwezo wa kuhudhuria katika mahakama za nchi husika katika mashauri yeyote yanayoihusu Jumuiya.



Maofisa wengine na Watumishi wa Sekretarieti Jumuiya itakuwa pia na maofisa wengine na watumishi wa sekretarieti. Hawa wataojiriwa kwa mikataba, na masuala ya mishahara yao na muundo wa kazi vitashughulikiwa na Baraza la Mawaziri. Wafanyakazi hawa wote watakuwa na kinga ya kidiplomasia ya kushtakiwa.

Shughuli za Sekretarieti kwa Ujumla

Kwa ujumla, Sekretarieti ina majukumu mengine kadhaa kama ifuatavya:

- Kuandaa masuala ya kushughulikiwa na Baraza la Mawaziri na Bunge.
- Kupanga na kuratibu njia bora zaidi za kufikia makusudia na programu za Jumuiya
- Kufanyia uchanguzi jambo lolote linalaelekea kudhoofisha shughuli za Jumuiya
- Kusambaza habari kuhusu shughuli za Jumuiya
- Kufanya shughuli za utawala na mambo ya fedha.

2.1.5 SURAYA ISHIRINI NA NANE: MASUALA YA FEDHA

Kipengele cha fedha kinahusisha masuala ya bajeti na matumizi ya Jumuiya. Hii ni pamoja na ukaguzi wa mahesabu ya matumizi ya fedha. Zaidi ya hapa, lipo suala la kutengeneza kanuni za fedha. Kipengele cha fedha kitahusisha pia vyanzo vya mapato ya fedha na raslimali nyingine za Jumuiya.

Vyanzo vya Fedha

Vyanzo vya fedha za Jumuiya vitakuwa ni pamoja na michango sawa ya Nchi Wanachama. Pia, vyanzo vingine vitakuwa ni ruzuku kutoka kwa wafadhili wa

Jumuiya wa Kimataifa. Patakuwa pia na miradi, programu na misaada ya kiufundi pamoja na mapato yatakayotakana na shughuli za Jumuiya.

Bajeti

Itakuwa ni wajibu wa Katibu Mkuu kuandaa bajeti. Bajeti hii itajadiliwa na Baraza la Mawaziri na itapitishwa na Bunge. Bajeti itakuwa katika dola za Kimarekani. Mwaka wa fedha utakuwa ukianzia tarehe 1 Julai hadi tarehe 30 Juni ya mwaka unaofuata.

Ukaguzi wa Hesabu

Ukaguzi wa mahesabu utafanywa na Tume maalumu. Tume hi itaundwa na wakaguzi wakuu toka Nchi Wanachama.

Tume ya ukaguzi itafanya udhibiti wa miahango, vyanzo vya pesa na matumizi ya Jumuiya.

Tume hii haitapewa maelekezo wala kudhibitiwa na mtu yeyote.

3. USHIRIKIANO KATIKA UCHUMI, BIASHARA NA MALIASILI

3.1 SURA YA KUMI NA MOJA: USHIRIKIANO KWENYE ULEGEZAJI MASHARTI NA MAENDELEO YA BIASHARA.

Sura ya kumi na moja inajumuisha Ibara ya 74 mpaka Ibara ya 78.

Ibara hizi zinahusu kuanzishwa kwa sera ya biashara ya Afrika Mashariki, ushirikiano katika ulegezaji masharti, Muungano wa Forodha na Soko la Pamoja la biashara la Afrika Mashariki. Nchi Wanachama zitaanzisha Soko la pamoja baina yao.

Ndani ya soka hilo kutakuwa na uhuru wa kuhamia katika Nchi yoyote Mwanachama kwa wafanya kazi, huduma, bidhaa, mtaji na haki ya kudumu Uanzishwaji wa Soko la Pamoja utakuwa wa awamu na kufuatana na ratiba iliyothibitishwa na Baraza la Mawaziri ambalo linaweza kuweka vyombo na kuvipa madaraka na mamlaka ya kuongoza Soko la Pamoja kama linavyoona inafaa.

3.1.1 SURA YA KUMI NA MBILI: USHIRIKIANO KATIKA UWEKEZAJI NA MAENDELEO YA VIWANDA

Sura hii inahusisha Ibara ya 79 na 80.

Ibara ya 79 inazungumzia maendeleo ya viwanda. Ukuzaji wa viwanda utakuwa wa kujitosheleza na wenye uwiano. Nguvu ya ushindani ya sekta ya viwanda itaongezwa ili kuimarisha upanuzi wa biashara ya bidhaa za viwandani ndani ya Jumuiya na uuzaji nje wa bidhaa za viwandani toka Nchi Wanachama ili kufanikisha mageuzi ya mfumo wa uchumi utakaosukuma maendeleo ya jumla ya kiuchumi na kijamii katika Nchi Wanachama. Maendeleo ya wafanya biashara wadogowadogo wenyeji yatahimizwa pia.

Ibara ya 80 inazungumzia mikakati na maeneo yatakayaanza kushughulikiwa.

Nchi Wanachama zitachukua hatua za kuanzisha mkakati wa Viwanda vya Afrika Mashariki. Zitakuza mwingiliano wa uzalishaji baina ya viwanda vyenye kutoa bidhaa maalum zinazotumiwa na viwanda vingine katika uzalishaji. Lengo litakuwa ni kuimarisha na kusambaza matokea ya ukuaji wa viwanda na uenezaji wa teknolojia.

Hatua nyingine zitakazochakuliwa ni pamoja na kuendeleza viwanda vidogo na vya wastani, kusaidia maendeleo ya viwanda vya vifaa vya msingi vya kuzalishia mali na vya kuzalisha bidhaa zinazotumiwa na viwanda vingine katika kuzalisha mali kwa kusudi la kupata faida za uchumi uliopanuka; kuinua utafiti na maendeleo ya viwanda; kuanzisha na kurekebisha vivutio vya vitega uchumi; kusambaza habari za viwanda na teknolojia ; pamoja na kuepuka utoaji wa kadi mara mbili.

3.1.2 SURA YA KUMI NA NNE: USHIRIKIANO KATIKA HAZINA YA SERIKALI NA FEDHA

Sura hii inajumuisha Ibara ya 82 mpaka Ibara ya 85.

Ibara ya 82 inahusu upana wa ushirikiano. Nchi Wanachama zinakubali kushirikiano katika masuala ya fedha na kudumisha ubadilishaji wa fedha kama msingi wa kuanzishwa kwa fedha za aina moja. Zitaainisha sera zao kuu za kiuchumi hasa katika sera za viwanda vya kubadilishana fedha, sera ya viwango vya riba, na sera za hazina ya serikali. Zitaondoa vikwazo vyote ili kuruhusu usafirishaji huru wa bidhaa, huduma, na mtaji katika Jumuiya



Zitadumisha pia ubadilishaji wa sarafu zao uliopo ili kukuza matumizi ya sarafu za taifa katika kufanya malipo miongoni mwa Nchi Wanachama na hivyo kupunguza matumizi ya fedha za kigeni. Zitachukua hatua zinazofaa zitakazokuza biashara na kuwezesha uhamishaji wa mitaji katika Jumuiya. Mwishowe zitaunganisha mifumo ya kifedha ya Nchi Wanachama.

Ibara ya 83 inahusu uainishaji wa sera za hazina za serikali na fedha. Nchi Wanachama zinakubaliana kuandaa masharti yote yanayohusiana na matumizi ya fedha za kigeni katika uingizaji na utaoji bidhaa katika Jumuiya; kudumisha viwango vya ubadilishaji huru wa fedha na kuimarisha kiwango cha akiba yao ya kimataifa. Zinakubaliana pia kurekebisha sera zao za hazina ya serikali na faida halisi ya

muamana kwa serikali ili kuhakikisha kuwapo kwa uimara wa fedha na mafanikio kwenye ukuaji wa uchumi wa kudumu. Zitaoinisha pia sera zao za kodi kwa lengo la kufuta kabisa upatashaji wa kodi ili kuleta mgawanyo wa raslimali wenye ufanisi katika Jumuiya.

Ibara ya 85 inahusu shughuli za benki na ukuza ji wa Soko la Mtaji.

Nchi Wanachama zimekubaliana kutekeleza programu ya maendeleo ya Soko la mtaji katika Jumuiya ili kumudu mazingira yanayofaa kwa ajili ya uhamishaji wa mtaji katika Jumuiya. Katika kutimiza lengo hili Nchi Wanachama zinatakiwa kukuza matumizi ya fedha katika uendeshaji wa mifumo ya uchumi ya kanda chini ya mfumo wa Soko huria.

Zinatakiwa pia kuainisha sheria zao za shughuli za benki; kuainisha mifumo ya kanuni za sheria na miundo ya urekebishaji; kuainisha na kutengeneza viwango sawa vya taratibu za masoko; na kuainisha sera zinazaothiri masoko ya mtaji, hasa utaoji wa motisha kwa ajili ya maendeleo ya masoko ya mtaji katika eneo hili. Hatua nyingine ni pamoja na kuanzisha Soko la hisa la kikanda katika jumuiya lenye matawi katika kila Nchi Wanachama, na kuweka hatua za kuzuia vitendo vya uhamishaji fedha usio halali.

Ibara ya 86 inahusu uhamishaji wa mtaji. Nchi Wanachama zitaruhusu uhamishaji huru wa mtaji wa ndani ya jumuiya, kuendeleza, kuainisha na mwishowe kuunganisha mifumo yao ya kifedha kulingana na ratiba itakayopangwa na Baraza la Mawaziri.

Kwa kuzingatia hila Nchi Wanachama zitahakikisha kwamba kuna uhuru wa mtiririko wa mtaji katika jumuiya kwa kuondoa udhibiti katika uhamishaji wa mtaji baina ya Nchi Wanachama; zitaruhusu raia na watu wanaoishi ndani ya Nchi Mwanachama kuwa na hisa na amana nyingine au kuwekeza kwenye shughuli zozote kwenye Nchi nyingine Mwanachama na kuhimiza biashara ya amana baina yao.

Ibara ya 87 inahusu ugharamiaji wa Miradi ya Pamoja. Nchi Wanachama zinakubali kushirikiano katika kugharamia miradi kwa pamoja katika kila nchi hasa ile inayoendeleza ushirikiano ndani ya Jumuiya. Zinakubaliana pia kushirikiana katika kuhamasisha mitaji ya kigeni kwa ajili ya kugharamia miradi ya kitaifa na ile ya pamoja.

3.1.3 SURA YA KUMI NA SABA: UHAMAJI HURU WA WATU, NGUVUKAZI, HUDUMA NA HAKI YA KUANZA MASKANI NA MAKAZI

Sura hii ina Ibara moja tu, yaani Ibara ya 104.

Yenyewe inahusu upana wa ushirikiano. Nchi Wanachama zinakubaliana kuchukua hatua za kuruhusu uhamiaji wa watu, nguvukazi na huduma na kuhakikisha kuwa watu wanapewa haki ya maskani na makazi ya muda popote ndani ya Jumuiya. Katika kutekeleza lengo hilo, Nchi Wanachama zitalegeza masharti ya kuvuka mpaka kwa raia wa Nchi Wanachama; zitakuwa na hati rasmi za kusafiria zinazafanana kwa raia wake; zitakubaliana kufungua vituo vya mpakani na kuviweka wazi kwa saa ishirini na nne na kuwa na sera za pamoja za uajiri.

Hali kadhalika, zitaainisha sera, pragramu na sheria za kazi pamoja na zile za afya na usalama wa wafanyakazi; zitaanzisha vituo vya kanda kwa ajili ya kuendeleza tija na ajira, na kubadilishana taarifa kuhusu upatikanaji wa ajira; zitaruhusu vituo vyao vya mafunzo kutumiwa na raia wa Nchi zote Wanachama; na zitahimiza shughuli za vyama vya waajiri na vya wafanyakazi kwa nia ya kuviimarisha..

3.1.4. SURA YA KUMI NA NANE: KILIMO NA UHAKIKA WA CHAKULA

Sura ya 18 inajumuisha Ibara ya 105 mpaka ya 110.

Ibara ya 105 inahusu upea na madhumuni ya ushirikiano katika sekta ya Kilimo, ambayo ni pamoja na kupata uhakika wa chakula kwa kuzingatia umuhimu wa uzalishaji wa mazao ya chakula ndani ya Jumuiya. Madhumuni haya yanalenga kuwepo kwa sera ya pamoja ya kilimo, utoshelevu wa chakula ndani ya jumuiya, ongezeko katika uzalishaji wa mazao, mifugo, uvuvi na misitu, hifadhi na utunzaji wa mavuno.

Nchi Wanachama zinakubaliana kushirikiano katika uainishaji wa sera za kilimo za Nchi Wanachama; uendelezaji wa uhakika wa chakula ndani ya Nchi Wanachama, utabiri wa hali ya hewa unaohusu kilimo, kuendeleza na kutumia mafunzo, utafiti na huduma za ushauri wa kilimo,




uanzishaji wa pragramu za pamoja kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya wanyama na mimea pamoja na wadudu waharibifu, uuzaji wa chakula na upashanaji habari juu ya uuzaji nje na uingizaji wa bidhaa za kilimo na hatua za pamoja za kupambana na ukame na tishio la jangwa.

Ibara ya 106 inaweka bayana masuala ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu. Nchi Wanachama zinakubaliana kuimarisha ushirikiano katika ukuzaji wa mbegu bora kwa njia ya utafiti na uzalishaji wa mimea; kukuza uwezo katika teknolojia ya uzalishaji mbegu; kuanzisha na kutunza hifadhi ya mbegu za tahadhari; kuainisha sera za mbegu; na kuandaa mazingira bora ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu kwa kutumia sekta binafsi.

Ibara ya 107 inahusu uzalishaji na usambazaji wa mifugo. Nchi Wanachama zitatayarisha utaratibu wa kushirikiana katika uzalishaji mitamba na vituo vya kuzalishia mitamba; zitahimiza ubadilishanaji wa bidhaa za aina ya mbegu ili kupanua msingi wa uendelezaji wa mifugo na zitahimiza ushirikishwaji wa sekta binafsi katika uzalishaji wa mifugo, biashara ya mbegu, mifugo ya mbegu, dawa na chanjo. Nchi Wanachama zitashirikiana pia katika uanishaji wa sheria za karantini katika uzazi wa chapa na vituo vya uzalishaji mifugo.

Ibara ya 108 ni juu ya udhibifi wa magonjwa ya mimea na wanyama. Nchi Wanachama zinakubaliana kuainisha sera, sheria na kanuni za kusimamia udhibiti wa wadudu waharibifu na magonjwa; kuainisha na kuimarisha taasisi za kusimamia sheria; kuainisha na kuimarisha wakaguzi na uthibitisha wa afya ya wanyama na za mimea; kujenga maobara za afya za wanyama na za mimea za Kanda; kushughulikia dalili na utambuzi wa wadudu waharibifu na magonjwa; kutumia taratibu za aina moja za kuhakikisha usalama; uthabiti na ufanisi wa pembejeo za kilimo pamoja na kemikali, dawa na chanjo, na kushirikiano katika mikakati ya kulinda, kutafuta dalili na

kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa ya wanyama walio ndani ya mipaka yao.



Ibara ya 109 inahusu umwagiliaji na ushughulikiaji wa vyanzo vya maji. Nchi Wanachama zinakubali kushirikiana katika kuandaa na kutekeleza programu za umwagiliaji za kitaifa na za Jumuiya; kuendeleza na kuhifadhi mifumo ya jadi ya umwagiliaji maji, uendeshaji wa vyanzo vya maji, ikiwemo ukingaji wa maji ya mvua, na kukuza matumizi ya mbinu salama kwa mazingira na matumizi ya ardhi.

Ibara ya 110 inahusu uhakika wa chakula. Nchi Wanachama zitaanzisha utaratibu wa kubadilishana taarifa juu ya mahitaji na ziada za ugavi, utabiri wa hali ya hewa na hali ya lishe na chakula; zitaoinisha ubora wa viwango vya pembejeo na mazao pamoja na viungo vya chakula; zitaendeleza njia za kupata taarifa juu ya bei za bidhaa katika Soko kwa wakati unaotakiwa; zitaanzisha na kutunza hifadhi za chakula cha akiba na zitaendeleza kilimo cha mimea ya baharini na maji baridi pamoja na ufugaji wa samaki.

3.1.5 SURA YA KUMI NA TISA: USHIRIKIANO KWENYE MAZINGIRA NA MALIASILI

Sura ya 19 inajumuisha Ibara ya 111 mpaka Ibara ya 114.

Ibara ya 111 inahusu masuala ya mazingira na maliasili. Pamoja na kutambua mchango wa mazingira safi katika kuleta maendeleo, Nchi Wanachama zinakubaliana kuchukua hatua za kuendeleza ushirikiano katika usimamizi wa pamoja na matumizi bora ya maliasili ndani ya Jumuiya. Zinakubaliana pia kutumia mikakati ya usimamiaji mazingira, kushirikiano na kuratibu sera pamoja na hatua za kulinda na kuhifadhi maliasili na mazingira dhidi ya aina zote za uhairibifu na uchafuzi unaotakana na shughuli za kimaendeleo.

Ibara ya 112 inahusu usimamizi wa mazingira. Nchi Wanachama zinakubaliana kuanzisha sera ya pamoja ya usimamizi wa mazingira ambayo itaendeleza mifuma ya kiteknolojia ya Nchi Wanachama, kuzuia, kusitisha na kugeuza madhara ya uchafuzi wa mazingira. Zinakubaliana pia kuchukua hatua za kudhibiti uchafuzi wa hewa, ardhi na maji nie ya mipaka kunakatakana na shughuli za maendeleo.

Ibara ya 113 inalenga katika uzuiaji wa biashara haramu na uhamishaji wa kemikali za sumu na uchafu wenye hatari. Nchi Wanachama zinakubaliana kushirikiana na kuwa na msimamo mmoja dhidi ya utupaji haramu wa kemikali za sumu na uchafu wenye hatari ndani ya jumuiya kutoka ama Nchi Mwanachama au nchi nyingine.

Ibara ya 114 inazungumzia usimamizi wa maliasili. Nchi Wanachama zinakubaliana kuchukua hatua za pamoja kuendeleza ushirikiano kwenye usimamizi wa pamoja na madhubuti na kuendeleza matumizi ya maliasili ndani ya Jumuiya kwa manufao ya pande zote za Nchi Wanachama. Mkazo utakuwa katika kuweka kanuni za pamoja kwa ajili ya kulinda rasilimali za majini na zile za nchi kavu wanazochangia.

3.1.6 SURA YA ISHIRINI: USHIRIKIANO KWENYE USIMAMIZI WA UTALII NA WANYAMA PORI

Sura ya 20 inajumuisha Ibara ya 115 mpaka Ibara ya 116.

Ibara ya 115 inahusu utalii. Nchi Wanachama zinakubaliana kuanzisha utaratibu wa pamoja na kuwasiliana baina yao katika kukuza na kutangaza utalii wenye kuleta kipato kikubwa kwa Jumuiya kwa idadi ndogo ya watalii. Nchi Wanachama zitafahamishana juu ya sera zao za utalii na kuanzisha muundo wa ushirikiano katika sekta hii ambao utahakikisha ugawanaji wa haki wa mafao baina ya Nchi Wanachama.

Mbali na kuanzisha kanuni za pamoja kwa kampuni za kiserikali na za binafsi zinazoshughulikia utalii na usafiri ili kusanifisha daraja za mahoteli na kuanzisha viwango vya kitaalamu vya mawakala wa utalii na usafiri katika Jumuiya. Nchi Wanachama zinaazimia kuendeleza mkakati wa kikanda wa kukuza utalii ambapo jitihada za nchi mojamoja zitaimarishwa na nguvu za kikanda.

Ibara ya 116 inahusu usimamizi wa wanyama pori. Nchi Wanachama zitaanzisha sera na utaratibu wa pamoja kwa ajili ya hifadhi na utumiaji wa kudumu wa wanyamapori katika Jumuiya. Mkaza utawekwa katika kuunda sera za pamoja za hifadhi ya wanyama pari ndani na nie ya maenea yaliyahifadhiwa; kubadilishana hatari na kuwa na sera zinazafanana juu ya usimamizi na maendeleo ya wanyama pari; kuratibu juhudi za kudhibiti na kufuctilia vitenda vya uangili; kuhimiza matumizi ya pamoja ya vitua vya mafunza na utafiti na kuanzisha mipanga ya pamoja ya usimamizi wa maenea yaliyahifadhiwa yanayavukc mipaka ya nchi maia; na kuchukua hatua za kuridhia au kuingia na kutekeleza mikataba ya kimataifa inayohusika.

3.1.7 SURA YA ISHIRINI NA TANO: SEKTA BINAFSI NA RAIA

Sura ya 25 inajumuisha Ibara ya 127 mpaka Ibara ya 129.

Ibara ya 127 inahusu uwekaji wa mazingira yanayaruhusu sékta binafsi na raia. Nchi Wanachama zinakubaliana kuweka mazingira yanayaruhusu sekta binafsi na jamii kutumia kwa ukamilifu fursa inayotokana na kuundwa kwa jumuiya. Mkazo utawekwa katika kutoa nafasi kwa wafanyabiashara kushiriki kikamilifu katika kuboresha sera na shughuli za taasisi za Jumuiya ambazo zinawaathiri.


Nchi Wanachama zinaazimia pia kuboresha mazingira ya biashara kwa kujenga taratibu za uwekezaji, kulinda mali na haki na utaratibu mzuri wa sekta binafsi; kukuza maendeleo ya Soko kwa kuunganisha miundo mbinu na kuandaa vizuizi na vikwazo katika maendeleo ya Soko na uzalishaji; kurahisisha na kusaidia ubadilishanaji wa ujuzi na matumizi ya pamoja ya rasilimali pamoja na kuruhusu vitega uchumi kuvuka mipaka yao, na kuimarisha ushiriki wa mashirika yao ya biashara au ya vyama vya biashara katika uandaaji wa sera zao za uchumi kitaifa.

Ibara ya 128 inahusu uimarishaji wa sekta binafsi. Nchi Wanachama zimeamua kujitahidi kuanzisha pragramu ambazo zitaimarisha na kukuza utendaji wa sekta binafsi ili kuifanya iwe nyenzo ya kufanikisha maendeleo ya uchumi wa nchi zao. Ili kutimiza lengo hilo Nchi Wanachama zimekubaliana kuhimiza utumiaji wa rasilimali adimu iliyopo kwa ufanisi na kukuza maendeleo ya mashirika ya sekta binafsi yanayojihusisha na aina zote za shughuli za uchumi kama vile vyama vya wafanyabiashara na wenye viwanda, shirikisha la vyama vya wenye viwanda, kilimo, watengenezaji bidhaa, wakulima, na vikundi vya kutoa huduma na vikundi vya kitaalamu.

Ibara ya 129 inahusu ushirikiano kati ya mashirika ya biashara na vyombo vya kitaalamu. Nchi Wanachama zinakubaliana kushirikiana katika kuendeleza hatua za pamoja kuhakikisha kuwa zinaimarisha viungo vilivyopa kati ya mashirika yao ya biashara, vyama vya wafanyakazi na vya waajiri na vyombo vya kitaalamu.

Ushirikiano huu utakuzwa kwa kuunga mkana shughuli za pamoja ambazo zitakuza biashara na uwekezaji baina ya Nchi Wanachama, kutambua na kuchangia kwa ajili ya utendaji bora wa ushirikiano baina ya mashirika ya

biashara, vikundi vya kitaalamu na kibiashara na vyama vya aina hiyo ndani ya Jumuiya; na kuhimiza na kukuza utaoji wa maamuzi yanayafaa ya Baraza la Mawaziri na taasisi nyingine za jumuiya katika maeneo yanayagusa sekta binafsi, na kusimamia utekelezaji wa maamuzi haya.





4. HUDUMA, VIWANGO NA MASUALA YA KIJAMII

4.1 SURA YA KUMI NA TANO: USHIRIKIANO KATIKA MIUNDOMBINU NA HUDUMA

Sura hii inajumuisha Ibara ya 89 hadi 101.

Ibara ya 89 inahusu sera za pamoja za Usafiri na Mawasiliano. Katika kuendeleza mshikamano, Nchi Wanachama zinakubaliana kuanzisha sera za pamoja za usafiri na mawasiliano. Hatua kadhaa zitachakuliwa ili kuwezesha mwingiliano mkubwa wa watu, bidhaa na huduma ndani ya Jumuiya. Hatua hizi ni pamoja na kuanzisha viwango na sheria zilizolingana; kujenga, kutunza, kupandisha hadhi, kukarabati na kuunganisha barabara, njia za reli, viwanja vya ndege, mabamba na bandari kwenye nchi zao.

Zitapitia na kusanifu upya aina za mifumo ya usafiri baina yao na kuanzisha njia mpya ndani ya Jumuiya kwa ajili ya kusafirisha aina za bidhaa na huduma zinazozalishwa kwenye Nchi Wanachama. Zitatunza, kupanua na kupandisha hadhi huduma za mawasiliano ili kuboresha mahusiano kati ya watu na wafanyabiashara katika Nchi Wanachama. Zitaendeleza matumizi kamili ya masoko na nafasi za kuwekeza zitakazoundwa na Jumuiya. Zitatao nafasi maalumu ya upendeleo kwa Nchi Wanachama zisizopakana na bahari kwa kutumia vipengele vilivyomo kwenye Sura hii.

Nchi Wanachama zitatoa pia ulinzi na hifadhi kwa mifumo ya usafirishaji ili kuhakikisha kuwa kuna usafirishaji salama wa bidhaa na watu ndani ya Jumuiya;


zitachakua hatua zinazakusudia kuainisha na kutumia kwa pamoja nyenza na pragramu katika vyombo vyao vya kitaifa vilivyapa kwa ajili ya mafunza ya wafanyakazi katika uwanja wa usafirishaji na mawasiliano. Hatimaye zitabadilishana taarifa ya maendeleo ya teknolojia katika usafirishaji na mawasiliano.

Ibara ya 90 inahusu Barabara na Usafiri wa Barabara. Nchi Wanachama zitachukuwa hatua ya kuridhia au kuingia katika mikakati ya kimataifa inayohusu usafiri wa barabara. Zitaainisha sheria zao za usafiri, kanuni na sheria za barabara pamoja na utoaji leseni na mafunzo kwa madereva. Zitakubaliana juu ya masharti ya pamoja kwa ajili ya kuweka bima za magari na mizigo. Zitatoa masharti ya msingi ya kiusalama kuhusiana na ufungaji wa mizigo, upakizi pamoja na usafirishaji wa vitu vya hatari.

Ibara ya 91 inahusu Reli na Usafiri wa Reli. Nchi Wanachama zinakubaliana kuanzisha na kudumisha huduma za reli zitakazoratibiwa kwa pamoja na ambazo zitaunganisha Nchi Wanachama kwa ufanisi. Kwa pamoja zitapitisha sera kwa ajili ya maendeleo na utengenezaji wa vifaa na zana za reli na usafiri wa reli ili kuzifanya reli zao kuwa na ufanisi zaidi na za ushindani.

Zitachukua hatua za kurahisisha na kuainisha usafiri wa reli ndani ya Jumuiya. Zitaainisha taratibu zinazahusiana na ufungaji wa mizigo, utiaji alama na upakizi wa mizigo kwenye mabehewa ya treni kwa ajili ya kusafirishwa ndani ya Jumuiya. Zitakubaliana kutaza ushuru usikuwa na ubaguzi kwa bidhaa zinazosafirishwa kwa treni ndani ya Jumuiya na kuhakikisha kuna utendaji wa hali ya juu.

Ibara ya 92 inahusu Usafiri wa Anga na Usafiri wa Ndege za Kiraia. Nchi Wanachama zitaainisha sera zao zinazohusu usafiri wa anga ili kuendeleza usafiri. Zitachakua hatua zinazostahili kuwezesha uanzishaji wa huduma za matumizi bora ya ndege kama hatua za kuimarisha usafiri wa anga katika Jumuiya. Zitaainisha sera za pamoja kuanzisha usafiri wa anga wa kiraia katika jumuiya kwa kushirikiano na mashirika mengine ya kimataifa. Zitakusanya huduma za usafiri wa anga madhubuti na zenye faida kwa kuziendesha kwa njia huru. Vilevile zitalegeza masharti ya utaoji wa haki ya usafiri kwa abiria na mizigo kwa lengo la kuongeza ufanisi na faida kwa mashirika yao ya ndege. Zitaainisha sheria na kanuni za usafiri wa anga kufuatana na Mkataba wa Kimataifa wa Chicago, hasa ambatisho namba tisa la sera za Chama cha Kimataifa cha Usafiri wa Anga (IAAO). Zitaifikiria njia za kuanzisha, kudumisha na kuratibu huduma zao za uongozaji wa ndege, mawasiliano na utabiri wa hali ya hewa.



Ibara ya 93 na 94 zinahusu Usafiri wa Baharini na Bandari, na Usafiri wa Majini wa Bara

Nchi Wanachama zitaanzisha sera na mifumo ya pamoja ya usafiri wa majini. Zitaanzisha huduma za bandari madhubuti kwa kubinafsisha na kuziendesha kibiashara. Zitaridhia au kuingia mikataba ya kimataifa ya usafiri wa baharini; ushirikiano katika miradi ya pamoja, ukarabati wa vifaavya mawasilialiana, usalama katika huduma za usafiri wa njia za majini za bara, na zitaainisha gharama za usafiri na uchukuzi.

Ibara ya 95 inahusu usafiri wa aina mbalimbali Nchi Wanachama zitaoinisha na kurahisisha kanuni, taratibu na nyaraka zinazatakiwa kwa usafiri wa aina mbalimbali katika jumuiya.

Ibara ya 97 inahusu Wasafirisha mizigo, Mawakala wa faradha na mawakala wa meli. Nchi Wanachama zitaainisha masharti ya usajili na utaoji leseni kwa wasafirishaji mizigo, mawakala wa utaoji mizigo na wa meli. Zitamruhusu mtu yeyote kusajiliwa na kupewa leseni kama msafirishaji mizigo, wakala wa kukomboa mizigo na wa meli, ili mradi mtu huya anatemiza masharti ya kisheria. Hazitaweka vizuizi kwenye shughuli za kibiashara, haki na wajibu wa msafirisha mizigo ama wakala wa usafirishaji mizigo aliyesajiliwa na kupewa leseni kisheria.

Ibara ya 98 na 99 zinahusu Huduma za posta na simu. Nchi Wanachama zitaongeza ushirikiano wa mashirika yao ya posta na kubuni njia na mbinu za kupata huduma za posta za haraka, za kuaminika, salama, zenye faida na zinazofanya kazi vizuri baina yao. Zitaimarisha vituo vya uchambuzi wa barua, njia za utumaji, usafirishaji na usambazaji wa barua ndani ya Jumuiya. Zitachangishana fedha, rasilimali za kiufundi na wafanyakazi kwa ajili ya kuboresha huduma za posta. Zitapanua Soko litakalohimili ushindani na kuanzisha mifumo mipya ya mafunzo kwa wafanyakazi wa jumuiya, kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa, itaboresha na kudumisha mawasiliano ya simu inayozuiunganisha Nchi Wanachama na kutafuta vifaa vya kisasa. Zitaainisha na kutoza ushuru bila kubagua. Itakarabati vifaa vya mawasiliano na kujumuisha mafunzo na kubadilishana watendaji miongoni mwa wanachama.

Ibara ya 100 inahusu Huduma za Utabiri wa Hali ya Hewa. Kila Nchi Mwanachama itakusanya na kueneza kwenye Nchi nyingine Wanachama taarifa za utabiri wa hali ya hewa ili kurahisisha utendaji bora wa usafiri wa anga. Kwa hivyo mtandao wa vyombo vya utabiri wa hali ya hewa na mawasiliana utapanuliwa na kuboreshwa. Hali kadhalika mafunzo na uchunguzi. katika vituo vya utabiri wa hali ya hewa utaimarishwa.

Nchi Wanachama zitashirikiana na kusaidiana katika shughuli zote za Shirika la Utabiri wa Hali ya Hewa la Dunia (WMA) zinazoathiri maslahi ya jumuiya hususan ufuatiliaji wa mabadiliko ya kiana na ya kihali ya hewa ya ulimwengu na zitabadilishana taarifa ya ubingwa kuhusu maendeleo mapya katika sayansi ya utabiri wa hali ya hewa na teknolojia pamoja na vipimo na ulinganishaji wa zana mbalimbali.

Ibara ya 101 inahusu nishati. Nchi Wanachama zitaanzisha sera na taratibu za kukuza matumizi, maendeleo, utafiti wa pamoja na matumizi ya rasilimali mbalimbali za nishati zinazapatikana ndani ya ukanda huu.

4.1.1 SURA YA KUMI NA SITA: USHIRIKIANO KATIKA MAENDELEO YA WATU , SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Sura hii ina Ibara za 102 na 103.

Ibara ya 102 inahusu elimu na mafunzo. jumuiya itakuza ushirikiano katika maendeleo ya elimu na mafunzo kwa kuratibu sera na programu za maendeleo ya watu na kuimarisha taasisi za utafiti. Shughuli za Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika ya Mashariki zitaimarishwa na wasomi kuhimizwa pamoja na kukaribisha sekta binafsi kutoa elimu. Mitaala, mitihani, vyeti na hadhi ya vyuo vitaoinishwa ili kuleta usawa.

Ibara ya 103 inahusu Sayansi na, Teknolojia. Kwa kutambua umuhimu wa msingi wa sayansi na teknolojia katika maendeleo. ya uchumi, Nchi Wanachama zinakubali kukuza ushirikiano kwenye maendeleo ya sayansi na teknolojia ndani ya Jumuiya. Lenga hili litatekelezwa kwa uanzishwaji na usaidizi wa pamoja wa utafiti wa kisayansi na wa kiteknolojia na wa afisi za fani mbalimbali za sayansi na teknolojia; na uainzishaji wa mazingira yanayafao kwa ajili ya kuendeleza sayansi na teknolojia katika jumuiya.

Ushirikiano huu utaendelezwa pia kwa uhimizaji wa matumizi na uendelezaji wa sayansi na teknolojia katika jumuiya; uhamasishaji wa misaada ya kiufundi na ya kifedha kutaka ndani na nje ya Jumuiya na kutaka kwenye mashirika au mawakala wa kimataifa kwa ajili ya kuendeleza sayansi na teknolojia katika jumuiya; kubadilishana taarifa za kisayansi, watumishi pamoja na ukuzaji na uchapishaji wa matakeo ya utafiti.

Hatua nyingine zitakazochukuliwa ni pamoja na Ushirikiano katika kuwakua wafanyakazi wa nyanja mbalimbali za kisayansi na kiteknolojia katika viwango vyote kwa kutumia taasisi zilizopo na zilizoanzishwa hivi karibuni; kukuza, kuendeleza na kutumia taarifa za kiteknolojia na nyinginezo kwenye jumuiya nzima; kuanzisha miongazo ya pamoja ya maadili kwa ajili ya uchunguzi; na kuanzisha sera ya biashara ya teknolojia na kukuza na kulinda haki miliki.

4.1.2 SURA YA ISHIRINI NA MOJA: MASUALA YA AFYA, JAMII NA UTAMADUNI

Sura hii inajumuisha Ibara ya 117 mpaka Ibara ya 120.

Ibara ya 118 inahusu masuala ya afya. Katika ushirikiano wa masuala ya afya Nchi Wanachama zimekubaliana kuchukua hatua za pamoja kuzuia na kudhibiti magonjwa yanayoambukiza na yasiyaombukiza. Zitadhibiti maradhi, yanayaenea kwa haraka, magonjwa ya mlipuka, magonjwa sugu kama virusi vya UKIMWI, malaria, kipindupindu, homa ya manjano, ambayo yanaweza kuhatarisha afya katika Nchi Wanachama.

Nchi Wanachama zitashiriki katika kutoa huduma za chanjo kwa umma kwa afya ya jamii; kuanzisha sera ya pamoja ya dawa kwa kudhibiti viwango vya ubora; kukuza utafiti, kuendeleza mafunzo na kubadilishana taarifa za afya, kuendeleza na kutangaza dawa na vyakula vya asili na lishe.

Ibara ya 119 inahusu utamaduni na michezo. Nchi Wanachama zitahimiza kuwapa kwa ushirikiano katika nyanja za utamaduni na michezo kwa kukuza na kuimarisha michezo, lugha za asili hasa Kiswahili kuwa lugha ya mawasiliano baina ya watu; na kuridhia mkataba, kanuni, sera ya biashara, ulinzi na hifadhi ya mali ya kitamaduni.

Ibara ya 120 inahusu Ustawi wa Jamii. Nchi Wanachama zinaozimia kushirikiano katika ajira, kuandaa umaskini na ujinga kwa kuwapa programu za mafunzo ya ufundi stadi, kuhesabu, kusoma na kuandika. Hali kadhalika zitaanzisha mtazamo wa pamoja wa kuyahudumia makundi ya wanyonge.

4.1.3 SURA YA ISHIRINI NA MBILI: KUIMARISHA NAFASI YA WANAWAKE KATIKA MAENDELEO YA KIUCHUMI NA KIJAMII

Sura hii ina ibara ya 121 na 122.

Ibara ya 121 inahusu Nafasi ya Wanawake katika Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii. Nchi Wanachama zinakubaliana kuwa wanawake wana mchango mkubwa sana katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Hivyo basi, zitawashirikisha wanawake kikamilifu katika pragramu za maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Zitakuza uwezo wa wanawake kwa kuwapa ajira ya kudumu, nafasi katika uangazi wa ngazi za juu za Maamuzi, kufuta sheria na kupinga mila na desturi zinazawabagua wanawake, kuandoa fikra patovu kuhusu wanawake na Hivyo kujenga usawa kati ya jinsia za wanawake na wanaume.

Ibara ya 122 inahusu Nafasi ya Wanawake katika biashara. Katika kutambua umuhimu wa wanawake kuwa kiungo muhimu cha uchumi kati ya kilimo, viwanda na biashara, Nchi Wanachama zinakubali kuongeza ushirikishwaji wa wanawake kwenye biashara katika kiwango cha kutunga sera na pragramu kwa ajili yao; kuandosha sheria zote, kanuni na matendo yanayomzuia mwanamke kupata msaada wa kifedha pamoja na mikopo; kuanzisha mikakati ya elimu ya kazi na mafunzo ya kiufundi ili kuboresha kipato; na kuunga mkono vyama vya ki-biashara vya wanawake vya ngazi mbalimbali.

5.MASUALA YA SIASA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

5.1. SURA YA ISHIRINI NA TATU: USHIRIKIANO KATIKA MASUALA YA KISIASA

Sura ya 23 inajumuisha Ibara ya 123 mpaka Ibara ya 125.

Ibara ya 123 inafafanao masuala ya kisiasa. Ili kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya jumuiya, Nchi Wanachama zitaanzisha sera za pamoja za masuala ya nje na usalama. Madhumuni ya sera za pamoja za nje na za usalama yatakuwa ni pamoja na kulinda maadili ya pamoja, manufao ya msingi na uhuru wa jumuiya, na kuimarisha usalama wa jumuiya na nchi zake Wanachama katika hali zote; kuendeleza na kuimarisha demokrasia na utawala wa sheria na kuheshimu haki za binadamu na uhuru wa masuala ya msingi.

Madhumuni mengine yatakayozingatiwa ni pamoja na kulinda amani na kuimarisha usalama wa kimataifa kati ya Nchi Wanachama na ndani ya jumuiya; kukuza ushirikiano katika vikao vya kimataifa; na hatimaye kuhimiza uanzishwaji wa Shirikisha la Kisiasa la Nchi Wanachama.

Madhumuni na malengo yote hayo yatafikiwa kwa kuanzisha mfumo wa ushirikiano kati ya Nchi Wanachama juu ya suala lolote la sera za nje au za usalama zenye manufao ya jumla katika jumuiya ili kupata msimamo wa pamoja utakaotumiwa na Nchi Wanachama; kufahamishana shughuli za Nchi Wanachama na kuzitetea kwenye mashirika na mikutano ya kimataifa, na kuunga mkono kikamilifu sera za nje na za usalama za jumuiya, na kujiepusha na kitendo chochote kwa upande wa Nchi Wanachama kinachokwenda kinyume na maslahi ya Jumuiya, au kile ambacho

kinaweza kuzorotesha uwezo wa jumuiya kama chombo cha pamoja katika masuala ya kimataifa.

Masuala mengine yatakayazingatiwa ni pamoja na kumaliza mitafaruku na migogoro kati na ndani ya Nchi Wanachama kwa amani, kufahamishana juu ya sera za ulinzi za Nchi Wanachama, na kukuza ushirikiano kati ya Mabunge ya Nchi Wanachama na Bunge la Jumuiya.

Ibara ya 124 inazingatia amani na usalama wa kikanda. Kwa kuzingatia kwamba amani na usalama ni mambo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Jumuiya, Nchi Wanachama zinakubaliana kuhimiza na kudumisha amani na usalama wa Nchi Wanachama kwa njia ya kuzuia, kuendesha vizuri na kumaliza migogoro na mitafaruku kati ya nchi hizo.

Nchi Wanachama zinakubaliana kukuza na kudumisha ujirani mwema kama msingi wa kukuza amani na usalama katika Jumuiya. Kwa - pamoja zitaonzisha vyombo vya kikanda vya kusimamia majanga ambavyo vitahusisha uendeshaji wa mafunzo, ushirikiano wa kifundi na misaada katika eneo hili la ushirikiano.

Pamoja na kukubaliana kuanzisha mbinu za pamoja za kushughulikia wakimbizi, Nchi Wanachama zitaimarisha ushirikiano katika kushughulikia uhalifu wa kuvuka mipaka yao, kupeana msaada katika mambo ya uhalifu pamoja na kukamata na kuwarudisha wahalifu makwao na kubadilishana taarifa za kitaifa za kupambana na vitendo vya uhalifu,

Katika kutimiza malengo haya, Nchi Wanachama zinadhamiria kuimarisha ubadilishanaji taarifa za uhalifu na taarifa nyingine za usalama baina ya vituo vya habari za uhalifu vya nchi zao; kuimarisha mapambano ya pamoja kama vile kuwasaka wahalifu na ulinzi wa pamoja ili kukuza usalama



mipakani; kuanzisha vyombo vya mawasiliano vya pamoja vya usalama katika mipaka; kutumia sheria ya mfumo wa Umoja wa Mataifa juu ya kusaidiana katika mambo ya uhalifu; kuwa na makubaliano juu ya kupambana na usafirishaji haramu wa dawa za kulevya; kuwa na mabadilishano ya ziara ya vyombo vya usalama; kubadilishana pragramu za mafunzo kwa watumishi wa usalama; na kuanzisha mbinu za pamoja za kushughulikia wakimbizi.

Ibara ya 125 inahusu ulinzi. Kwa lengo la kukuza amani, ulinzi na utulivu katika ujirani mwema, Nchi Wanachama zinakubaliana kushirikiana kwa karibu sana katika mambo ya ulinzi.

5.1.1 SURA YA ISHIRINI NA SITA: UHUSIANO NA MASHIRIKA MENGINE YA KIKANDA NA YA KIMATAIFA NA WAHISANI

Sura hii ina Ibara moja, yaani Ibara ya 130. Ibara hii inahusu mashirika ya kimataifa na Wahisani. Nchi Wanachama zinakusudia kuheshimu ahadi zao kwa mashirika mengine ya kitaifa na kimataifa ambayo nchi hizo ni wanachama. Mbali na kusesitiza hamu yao ya kuwapa Umoja wa Afrika, zinachukulia Jumuiya yao kama moja ya hatua za kufikia malengo ya mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Afrika.

Kwa nia ya kuchangia kufanikisha malengo ya Jumuiya, Jumuiya itashirikiano na mashirika mengine ambayo shughuli zao zinaendana na madhumuni ya Jumuiya. Nchi Wanachama zitaweka umuhimu maalumu kwenye kushirikiano na Umoja wa Mataifa, mashirika yake na mashirika mengine ya kimataifa, pamoja na wahisani wate wanaounga mkana madhumuni ya Jumuiya.

6. MENGINEYO

6.1 SURA YA ISHIRINI NA TISA: VIFUNGU VYA JUMLA, VYA MPITO NA VYA MWISHO

Ibara ya 136 inahusu Makao Makuu ya Jumuiya na ahsi nyingine: Makao Makuu ya Jumuiya yatakuwa Arusha, Tanzania.

Ibara ya 137 inahusu Lugha Rasmi ya Jumuiya. Lugha rasmi ya Jumuiya itakuwa Kiingereza. Lugha ya Kiswahili itaendelezwa kama lugha ya mawasiliano ya kawaida ya Jumuiya.

Ibara ya 144 inahusu Muda wa Mkataba. Mkataba huu ni wa kudumu.

Ibara ya 145 inahusu Kujitoa Uanachama Nchi Mwanachama inaweza kujitoa kwenye Jumuiya ili mradi Bunge la Nchi hiyo Mwanachama limeamua kwa azimia lililoungwa mkono na zaidi ya theluthi mbili ya wajumbe wote wenye haki ya kupiga kura, na baada ya kumpa taarifa ya maandishi ya miezi kumi na mbili

Katibu Mkuu juu ya dhamira ya kujitoa. Nchi Mwanachama inayotaka kujitoa kwenye Jumuiya itaendelea kuwajibika kutimiza majukumu yake chini ya mkataba huu katika miezi kumi na mbili ya taarifa ya kujitoa kwake.

Bila kujali kutimilika kwa kujitoa huko kwa uanachama wa Nchi kama hiyo baada ya kumalizika kwa muda wa taarifa, Nchi hiyo itabaki na wajibu wa kutimiza majukumu yake yote yaliyokuwapa na ya muda mrefu yaliyopitishwa wakati ikiwa Mwanachama.

Ibara ya 147 inahusu Kufukuzwa kwa Mwanachama

Mkutano wa Wakuu wa Nchi unaweza kuifukuza Nchi Mwanachama kutoka Jumuiya kwa ukiukwaji mkubwa na wa mara kwa mara wa kanuni na malengo ya mkataba huu baada ya kuipa Nchi Mwanachama hiyo notisi ya maondishi ya miezi kumi na mbili.

Baada ya kumalizika kipindi kiliahatajwa hapa juu, Nchi Mwanachama inayahusika itaendelea kuheshimu vifungu vya mkataba huu na kutakiwa kutekeleza majukumu yote yaliyabaki na majukumu ya muda mrefu iliyapewa wakati wa Uanachama.

Ibara ya 149 inahusu Haki juu ya miliki na mali ya Jumuiya baada ya kuacha uanachama. Pale Nchi Mwanachama inapojitoa au kufukuzwa kufuatana na Ibara za 145 na 147, miliki za Jumuiya zilizo katika Nchi Mwanachama hiyo zitabakia mikononi mwa Jumuiya. Nchi ambayo imeacha kuwa mwanachama wa Jumuiya haitakuwa na madau au haki yoyote juu ya mali za Jumuiya. Jumuiya itaendelea na wanachama waliobakia liacha ya kujitoa au kufukuzwa kwa Nchi yoyote Mwanachama.

Ibara ya 150 inahusu Urekebishaji wa Mkataba

Mkataba huu unaweza kurekebishwa wakati wowote kwa makubaliano baina ya Nchi zote Wanachama baada ya kupokea mapendekezo ya marekebisho kutaka Nchi yoyote Mwanachama au Baraza la Mawaziri.

Mapendekezo yoyote ya marekebisho ya Mkataba huu yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu kwa maandishi ambayo mnamo siku thelathini (30) za kupokea mapendekezo hayo, atawasilisha marekebisho yaliyopendekezwa kwa Nchi Wanachama. Nchi Wanachama zinazotaka kutoa maoni juu ya mapendekezo zitafanya hivyo katika kipindi cha siku tisini (90) tangu tarehe ya kutumiwa mapendekezo na Katibu Mkuu.

Baada ya muda huo (siku 90) kwisha, Katibu Mkuu atawasilisha mapendekezo pamoja na maoni yoyote yaliyopokelewa kutoka kwa Nchi Wanachama katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi kupitia Baraza la Mawaziri. Marekebisho yoyote ya Mkataba huu yatapitishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi, nayo yataanza kufanya kazi mara baada ya kuridhiwa na Nchi zote Wanachama.

Ibara ya 152 inahusu Utekelezaji wa Mkataba Mkataba huu utaanza kufanya kazi baada ya kukubaliwa na Nchi Wanachama na kukabidhi hati za maridhiana kwa Katibu Mkuu.

7. VIAMBATISHO

7.1 HATI ZA AWALI ZA MKATABA WA UANZISHAJI WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

Utangulizi

Hati za Awali za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni sehemu ya Mkataba ulioanzisha Jumuiya hiyo. Uhalali huu unafafanuliwa katika Ibara ya 151 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ifuatavya:

1. Nchi Wanachama zitakamilisha Hati za Awali kama zitakavyaona kuna umuhimu, katika kila eneo la ushirikiano ambazo zitaeleza wazi madhumuni na mawanda ya ushirikiano na namna ya kuendesha ushirikiano.
2. Kila Hati ya Awali itaidhinishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama baada ya mapendekezo ya Baraza la Mawaziri.
3. Kila Hati ya Awali itapaswa kutiwa sahihi na kuridhiwa na pande zote husika.
4. Viambatisha na Hati ya Awali za Mkataba huu zitakuwa ni sehemu ya Mkataba

Zifuataza ni baadhi ya Hati za Awali ambazo tayari zimekamilishwa na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Nchi Wanachama na kutiwa sahihi na pande zote husika mpaka Septemba 2001:

1. Hati ya Awali juu ya Usanifishaji na Uhakiki wa Ubora, Vipimo na Upimaji. (Ibara ya 81)
2. Makubaliano juu ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Madawa ya kulevya (Ibara ya 124, Kifungu cha 5 (e))
3. Makubaliano ya Pande Tatu juu ya Usafiri wa Barabara (Ibara ya 142, Kifungu cha 1(f))
4. Makubaliano ya Pande Tatu juu ya Usafiri wa Maji Baridi (Ibara ya 142, Kifungu cha (g))
5. Waraka wa Maelewano juu ya Ushirikiano katika Ulinzi (Ibara ya 142, Kifungu cha 1(e))
6. Waraka wa Maelewano juu ya Uratibu wa Sera ya Mambo ya Nchi za Nje (Ibara ya 142, Kifungu cha 1 (h))
7. Makubaliano ya Pande Tatu juu ya Kuepuka Ulipaji Kodi Maradufu na Kuzuia Kukwepa Kulipa Kodi ya Mapato (Ibara ya 142, Kifungu 1(d))
8. Hati ya Awali ya Uanzishaji wa Sekretariati ya Tume ya Kudumu ya Pamoja ya Ushirikiano baina ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, jamhuri ya Kenya na jamhuri ya Uganda (Ibara ya 142, Kifungu cha 1(b))
9. Waraka wa Maelewano baina ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Kenya na jamhuri ya Uganda kwa ajili ya Ushirikiano juu ya Usimamizi wa Mazingira (Ibara ya 142, Kifungu cha 1(l))
10. Makubaliano Yanayahusu Makao Makuu kati ya Sekretariati ya Tume ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Ibara ya 142, Kifungu cha 1(b))
11. Hati za Awali za Kufanya Maamuzi za: - Mkutano Mkuu wa Nchi (Ibara ya 11) - Baraza la Mawaziri (Ibara ya 18) - Kamati ya Uratibu (Ibara ya 18)

12. Vigezo vya Kukubaliwa Wanachama Wapya katika jumuiya ya Afrika Mashariki (Ibara ya 3, Kifungu cha 3)
13. Hati ya Awali ya Muundo wa Kitaasisi na Kisheria juu ya Uendelezaji wa Bonde la Ziwa Victoria

Nyaraka nyingine Muhimu

14. Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda wa Afrika Mashariki (Ibara ya 80)
15. Mkakati wa Maendeleo wa Afrika Mashariki kwa Kipindi cha 2001 – 2005
16. Ijue Jumuiya Mpya ya Afrika Mashariki - na George Nangale
17. Jumuiya ya Afrika Mashariki: Changamoto na Nafasi - Mhadhara Na. 1

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na:

Katibu Mkuu, Jumuiya ya Afrika Mashariki,
Sanduku la Barua, 1096, Arusha, Tanzania
Simu: 255-27-2504253 - 8, Faxi: 255-27-2504255
Barua pepe: eac@eachq.org
Web: <http://www.eachq.org>

7.1.1 BUNGE LA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI KATIKA KIKAO CHAKE CHA KWANZA – NOVEMBA 29 2001

JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA

1. Mh. Abdulrahman A. Kinana
[Spika - Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki]
2. Mh. Dk. Harrison Mwakyembe
3. Mh. George Francis Nangale
4. Mh. Balozi Isaac Abraham Sepetu
5. Mh. Saidi Bakari Jecha
6. Mh. Mabere Nyauchio Marando
7. Mh. Kate Sylvia Magdalen Kamba
8. Mh. Beatrice Matumbo Shelukindo
9. Mh. Mahfaudha Alley Hamid

JAMHURI YA UGANDA

1. Mh. Nanziri Sarah Bagalaaliwo
2. Mh. Richard Baker Ddudu [Capt.]
3. Mh. Sozi Kiwanuka Medi Kaggwa
4. Mh. Yanasani Bankobeza Kanyomozi
5. Mh. Mishambi Sheila Kawamara
6. Mh. Irene Ovonji Odida
7. Mh. Wandera Daniel Ogalo
8. Mh. Mutende Lydia Wanyoto
9. Mh. Muntu G. Mugisha [Maj. Gen.]

JAMHURI YA KENYA

1. Mh. Lt. Gen Abdullahi Aden
2. Mh. Haji Abdulrahim Haithar
3. Mh.. Prof. Margaret Kamar
4. Mh. Jared Benson Kangwana
5. Mh. Achieng Gilbert Mbeo
6. Mh. Calista Mwatela
7. Mh. Wairimu Rose Waruhiu
8. Mh. Mahamed Zubedi
9. Mh. Maxwell Shamalla

WAJUMBE MAALUM - (MAWAZIRI WA WIZARA ZINAZOHUSIKA NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI)

1. Mh. Jakaya Mrisho Kikwete [Mb.], Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Tanzania
2. Mh. James Wapakhabulo [Mb.],
Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano vwa Jumuiya], Uganda
3. Mh. Kipyator Nicholas Kiprono Biwatt EGH, [Mb.]
Waziri wa Biashara na Viwanda, Kenya

WAJUMBE MAALUM (SEKRETARIETI YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI)

1. Mh. Nuwe Amanyu Mushega, Katibu Mkuu
2. Mh. Wilbert T.K. Kaahwa
Mshauri wa Jumuiya katika masuala ya Sheria

7.1.2 MAHAKAMA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

1. Mh. Jaji Moijo Ole Keiuwala, RAIS WA MAHAKAMA
2. Mh. Jaji Joseph Mulenga, MAKAMU RAIS WA MAHAKAMA
3. Mh. Jaji Joseph Sinde Warioba
4. Mh. Jaji Augustine Ramadhani
5. Mh. Jaji Salomy Bbosa
6. Mh. Jaji Jackson Kasanga Mulwa

Kimetolewa na

FRIEDRICH EBERT STIFTUNG

Barabara ya Kawawa , Plot 397 S.L.P. 4472

Dar es Salaam Tanzania

Simu + 255 022 2668575/2668786

Fax + 255 022 2668669

[Email: festanzania@raha.com](mailto:festanzania@raha.com)

Watayarishaji

Dk. Mahammed Omar Maundi

Bi. Tatu Tua, Bw. Adelardus Kilangi,

Bw. Francis Imanjama Wahariri

Dk. Mahammed Amar Maundi

Bi. Claire Lwehabura

Mratibu

Dk. Mohammed Omar Maundi

Michoro

8w. Francis Imanjama

Usanifu

Petra's Maridadi Ltd.

ISBN 9987 22 036 3